# JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714 – 2175 TOLEO Na. 13 JANUARI – JUNI, 2023








**KUTOKA KWA MRAJIS**



*Dkt. Benson Ndiege, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)*

Ndugu wasomaji,

Niwakaribishe tena katika Jarida la Ushirika, Toleo la Kumi na Tatu, ambalo ni mfululizo wa Majarida yanayoandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) katika jitihada za kuelimisha na kuhamasisha Umma kuhusu masuala na hatua mbalimbali zinazofanyika katika kuimarisha Sekta ya Ushirika.

## TCDC NA MAFANIKIO YA KIBIASHARA AFRIKA MASHARIKI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 ikiwa na jukumu la kusimamia na kuhamasisha Maendeleo ya Sekta ya Ushirika nchini kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 8 (1) cha sheria hiyo.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika ikiwa ni Taasisi inayojitegemea imejikita katika Usajili wa Vyama vya Ushirika kwa makundi mbalimbali yanayojishughulisha na kazi mbalimbali zikiwemo Kilimo, Biashara, Madini, Uvuvi na kuhakikisha kuwa watu wote

wanaojishughulisha katika shughuli hizo wanajiunga na Vyama Vya Ushirika ili kuweza kupata fursa mbalimbali zinazopatikana kwa urahisi wakiwa katika Vyama vya Ushirika ikiwemo Mitaji, na pembejeo za kilimo zitakazowawezesha katika kufanikisha shughuli hizo.

Kwa upande wa kibiashara, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kufanya vizuri katika ngazi mbalimbali za vijiji, kata, wilaya, mkoa, kitaifa na kimataifa.Katika ngazi ya kimataifa, Tume inashirikiana na nchi za Afrika Mshariki ili kuweza kukuza zaidi soko la kibiashara.

Hivi karibuni tumeshuhudia ushiriki wa Tume katika Mkutano wa Fursa za Kibiashara na Masoko nchini Sudan ya Kusini. Mkutano ambao uliandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Sudani ya Kusini, kwa lengo la kujadili na kuunganisha fursa za biashara na masoko ya mazao baina ya nchi hizi mbili.

Tume kama mdau mkubwa wa Ushirika inashirikiana pia na wadau wengine wa Ushirika katika kuhakikisha kuwa shughuli za kiuchumi zinafanikiwa kwa kiwango kikubwa,hii inadhihirishwa na ushiriki wa wadau wengine katika mkutano huo wa kibiashara Sudan Kusini zikiwemo Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali ambazo ni pamoja na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Shirika la Bima la Taifa (NIC), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Tume ya Ushindani Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Shirika la Ndege Tanzania (ATC), Mamlaka ya Usimamizi wa Petroli Tanzania (PURA), VETA Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Kwa upande wa Sekta Binafsi, makampuni yaliyoshiriki mkutano huo ni Kampuni ya Tobage, Junaco na Kusa Investment pamoja na SUMA JKT.

## RAIS SAMIA AZINDUA MPANGO WA 'BLOCK FARMING' KATIKA PROGRAMU YA 'BBT'




*Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, mara baada ya kukata utepe katika uzinduzi wa 'Block Farming', katika eneo la Chinangali -Chamwino, Jijini Dodoma, tarehe 20 Machi, 2023*


*Vijana wanaojishughulisha na Mradi wa wa Kilimo cha Kisasa (Block Farming) wakiwa kwenye Uzinduzi wa Mradi wa 'Block Farming' Chinangali – Chamwino Jijini Dodoma tarehe 20 Machi,2023*

Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Jumatatu, Machi 20, 2023 amezindua Kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja (Block Farming) katika programu ya *Building Better Tomorrow* (BBT).

Uzinduzi huo umefanyika katika eneo la Chinangali, Chamwino, mkoani Dodoma ukiwa na lengo la kuwawezesha vijana kujikwamua kiuchumi.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo chini ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, imeandaa programu ya BBT mahususi kupambana na changamoto ya ajira nchini na kuwawezesha vijana kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Dkt. Samia amewataka vijana kutumia fursa iliyoandaliwa na Serikali kupitia mradi wa kilimo cha kisasa na biashara ili kujikomboa na tatizo la ajira nchini na kuhakikisha kuwainua vijana kiuchumi

## RAIS DKT. SAMIA ATAKA MSHIKAMANO KWA MASLAHI YA WAFANYAKAZI




*Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwapungia mkono wafanyakazi katika Maadhimisho ya MeiMosi yaliofanyika kitaifa mkoani Morogoro tarehe 01 Mei, 2023*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amevitaka Vyama vya Wafanyakazi kuendelea kuwa na ushirikiano wa pamoja ili kuwa na nguvu ya majadiliano yenye kujenga na kuboresha maslahi ya Wafanyakazi.

Akiongea wakati wa Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi 2023 Mkoani Morogoro. Rais amevitaka vyama vya Wafanyakazi 13 vilivyo katika Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi kuwa na ushirikiano utakaowezesha kuwa na nguvu ya majadiliano yatakayojadili hoja zitakazoleta maslahi bora ya Wafanyakazi.




*Watumishi wa TCDC wakiwa kwenye Maandamano katika siku ya Wafanyakazi Duniani (Meimosi) iliyofanyika Mjini Morogoro tarehe 01 Mei, 2023*

Rais Mhe. Dkt. Samia amesema Serikali itaendelea kuwekeza na kuvutia wawekezaji nchini ili kujenga uchumi utakaowezesha maslahi bora ya wafanyakazi kupatikana kwa kushirikiana na Vyama vya Wafanyakazi.

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema maombi mbalimbali yaliyowasilishwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), ikiwemo nyongeza za mishaharana kupandisha madaraja kwa watumishi yametekelezwa kwa asilimia 95.

## VYAMA VYA USHIRIKA VYATAKIWA KUSHIRIKI KUSAMBAZA MBOLEA KWA WAKULIMA



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mwenye Kofia Katikati) akizungumza wakati alipotembelea Ghala la kuhifadhi Mbolea za Kampuni hiyo akiwa kwenye ziara ya kukagua shughuli za Kilimo tarehe 15 Januari, 2023.*

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe ameagiza Vyama Vikuu vya Ushirika Mkoani Ruvuma kuanza kusimamia na kuratibu upatikanaji na usambazaji wa mbolea kwa wanachama na wakulima kwa ujumla.

Waziri Bashe ametoa agizo hilo tarehe 15 Januari, 2023 wakati wa ziara ya kikazi Mkoani Ruvuma alipokuwa akipokea taarifa ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo katika siku ya kwanza ya ziara ya siku mbili mkoani humo.

Mhe. Bashe amesema, Vyama Vikuu vya Ushirika Mkoani humo vimekuwa vinaratibu upatikanaji wa mbolea na pembejeo za Korosho, Tumbaku na Kahawa kwa wakulima; sasa wajipange waanze pia kusambaza mbolea za mazao mengine kama vile Mahindi, Soya na Mbaazi.

“Kuanzia mwakani nataka kuona vyama hivi vinaratibu upatikanaji wa mbolea za mazao

mengine ili wakulima waweze kupata mbolea kwa wakati na kwa urahisi kisha kuongeza tija katika uzalishaji," Waziri Bashe amesisitiza.

Aidha, Waziri Bashe ameziagiza Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kufanya kazi kwa kushirikiana na kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kupitia Vyama vya Ushirika. "Mkifanikiwa kupitishia Mbolea katika Vyama Vikuu sitegemei kusikia kelele kutoka kwa wakulima kuhusu mbolea na wakati Tume ya Maendeleo ya Ushirika mmesambaa kila mkoa," Waziri Bashe alisisitiza.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma, Mhe. Odo Mwisho amepongeza jitihada za Wizara za kuagiza Mbolea kuwafikia wakulima kupitia Vyama Vikuu vya ushirika na kusema kuwa itasaidia kupunguza usumbufu kwa mkulima mmoja mmoja kufuata mbolea katika vituo vilivyopo Mijini.

Amesema wakulima wanatoka maeneo ya mbali kufuata Mbolea kwa wakala wa usambazaji hali inayosababisha kutumia muda mwingi katika foleni ya ununuzi wa mbolea hiyo. Hivyo, anaamini ikipitia katika vyama vikuu kila mkulima atapata mbolea yake kwa muda sahihi na karibu na maeneo ya uzalishaji.

Pia, Mhe. Mwisho ameiomba Serikali katika mgao wa ujenzi wa maghala ishirini mapya mkoani Ruvuma ambao unategemea kuanza kujengwa hivi karibuni uweze kuzingatia uhitajiwa maeneo na si kurundika maghala maeneo ambayo hayana uhitaji.

“Yapo maeneo ambayo maghala yaliyopo yanajitosheleza, nakuomba Mheshimiwa Waziri katika ujenzi wa maghala hayo yajengwe sehemu ambazo kweli zinauhitaji ili kuepusha utitiri na mlundikano wa Maghala sehemu moja," amesema Mhe.Mwisho.

# BODI ZA VYAMA VYA USHIRIKA ZATAKIWA KUSIMAMIA IPASAVYO VYAMA VYAO



*Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika (Usimamizi na Udhibiti), Collins Nyakunga akiongea wakati wa Kikao cha Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika kilichofanyika Jijini Dodoma tarehe 17 January, 2023.*

Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika wametakiwa kusimamia ipasavyo Vyama Vyao ili mali za Wanaushirika ziweze kutumika kuwaletea maendeleo na kuvifanya Vyama hivyo kuwa endelevu na kuaminika kwa wadau wake.

Wito huo umetolewa na Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika (Usimamizi na Udhibiti), Collins Nyakunga, Januari 17, 2023 JIjini Dodoma katika kikao kazi cha pamoja kati ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC), Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama (COASCO), Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) na Vyama Vikuu vya Ushirika nchini.

Naibu Mrajis Nyakunga amewataka viongozi wa Vyama vya Ushirika nchini kuhakikisha kuwa vyama vyao pamoja na vyama vilivyoko chini yao vinaondokana na hali mbaya ya Ukaguzi na kuhakikisha vitabu vya mahesabu vinaandaliwa ipasavyo na kukaguliwa na wakaguzi wa nje.

"Tunatarajia mkitoka hapa mkirudi kwenye Vyama vya Ushirika mpate nafasi mapema kujadiliana na kutekeleza tutakachokubaliana hapa ili kuondokana na changamoto zinazopelekea kupata hati chafu kabla hatua zaidi kuchukuliwa," amesema Nyakunga.

Aidha, Nyakunga amesema kuwa ili kuondokana na changamoto zinazopelekea kupata Hati Chafu inabidi viongozi wa Vyama Vikuu vya Ushirika kutambua majukumu yao, kutambua kazi zao na kufanya kazi kwa kuzingatia miongozo ya Vyama vya Ushirika.

Vilevile katika kikao kazi hicho, wajumbe wamejadili kuhusu Taarifa ya jumla ya hali ya ukaguzi wa COASCO na mpango wa utatuzi wa dosari zilizobainika katika ukaguzi huo.

Sambamaba na hilo wajumbe wamejadili kuhusu kuimarisha mtaji wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro ili kuiwezesha kuwa Benki ya Taifa ya Ushirika, ambapo Naibu Mrajis amevitaka Vyama Vikuu vya Ushirika kuweka kipaumbele katika kununua Hisa za Benki hiyo.

"Tuangalie namna gani tutakavyoweza kuvitumia Vyama vya Ushirika hususan Vyama ViKuu vya Ushirika kuhakikisha ndani ya muda mfupi tunapata fedha za kutosha ili kuwa na mtaji toshelevu wa Bil.15 ambazo zitatuwezesha kupata usajili wa Benki ya kitaifa ambayo Makao yake Makuu yatakuwa Jijini Dodoma," amesema Nyakunga.

# SERIKALI YAAHIDI KUJENGA GHALA "ISOWELU AMCOS"



*Waziri wa Kilimo Mhe. Mhe. Hussein Bashe akizungumza na wanachama wa ISOWELU AMCOS katika kijiji cha Mtwango mkoani Njombe tarehe 17 Januari, 2023.*

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeahidi kujenga Ghala la kuhifadhi Viazi kwa Chama cha Msingi cha Ushirika "ISOWELU AMCOS" kilichopo mkoani Njombe.Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe ametoa ahadi hiyo tarehe Januari 17, 2023 wakati wa kikao baina yake na wakulima na wanachama wa ISOWELU AMCOS ambapo Chama hicho hakina ghala la kuhifadhi mazao na kusababisha wakulima kuuzia mashambani.

Waziri Bashe amesema AMCOS hiyo inapaswa kuwa ya mfano na sehemu ya AMCOS nyingine kujifunza kutokana na utendaji wake kuwa mzuri na kuonesha matokeo chanya.

"Unajua Benki kukipatia Chama cha Ushirika mkopo wa Shilingi Billionimoja inamaanisha chama hicho kiko vizuri sana katika utendaji wake na katika urejeshaji mikopo, ni vyama vichache vinaweza kuaminika kama ISOWELU AMCOS; Sasa inapaswa vyama vyote viiige mambo mazuri kama ya Ushirika huu wa ISOWELU," amesema Mhe. Bashe.

Waziri Bashe ameupongeza Ushirika wa ISOWELU AMCOS na kueleza wanachama

wake wanalima viazi na kuvuna gunia 210 kwa ekari moja na kueleza huu ndiyo Ushirika unaohitajika nchini. Aidha, Mhe. Bashe ameagiza Vyama Vikuu vyote vya Ushirika kusajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na kuwa wakala wa Mbolea ili kurahisisha huduma za upatikanaji wa Mbolea kwa wanachama wake.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, ametoa rai kwa ISOWELU AMCOS kuendelea kufanya kazi ya kuwahudumia wakulima kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria zinazosimamia Vyama vya Ushirika kwa uadilifu mkubwa.

“Mnafanya vizuri mmepata sifa nyingi na mtaendelea kupata sifa hizo sasa msilewe sifa mkaanza kufanya mambo ya ajabu mkaanza kuharibu sifa hizi ziwajenge na zisibomoe,” amesema Dkt. Ndiege.

Mrajis ameitaka ISOWELU AMCOS kujipambanua na kujihusisha na uzalishaji wa mazao mengine na hivyo kuendelea kuboresha maisha yao baada ya mauzo badala ya kujikita kwenye kilimo cha viazi pekee.

Aidha, Mrajis amewashauri viongozi wa Ushirika wa ISOWELU AMCOS kuendelea na mchakato wa kuwapatia wanachama wao Bima ya Afya ili wanachama wake waweze kupata huduma za matibabu wanapougua.

Kwa upande wake Meneja wa ISOWELU AMCOS, Chesco Ng’eve, amesema Ushirika umewalea na kuwasimamia vyema ndiyo maana wamekuwa ni AMCOS bora kutokana na kusikiliza na kufuata maelekezo ya viongozi.

# AMCOS ZA PAMBA ZATAKIWA KUSAJILI NA MAZAO MENGINE



*Waziri wa Kilimo Mhe.Hussein Bashe akitoa maelekezo kuhusu mfumo wa Usajili wa Mkulima "Mkulima Hub" akiwa na wataalam wa mfumo huo ofisini kwake Jijini Dodoma tarehe 01 February, 2023.*

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, amewataka Viongozi wa AMCOS za Pamba kusajili mazao mengine yanayolimwa na wakulima katika Mikoa inayolima zao la Pamba.

Mheshimiwa Bashe amesema wanaosajili wakulima wa Pamba ni lazima wasajili na wakulima wa mazao mengine yanayolimwa katika maeneo hayo ili iwape fursa wakulima kutambulika na kupata pembejeo.

Waziri Bashe ametoa kauli hiyo Februari 01, 2023 wakati akipitishwa katika Mfumo Mpya wa Mauzo ya Pamba wa Kidigitali, Jijini Dodoma.

Mhe. Bashe amesema kipindi hiki ambacho wanasubiri muda wa mavuno na minada, Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na TCDC na Bodi ya Stakabadhi za Ghala kuanza kupeleka vifaa na kuwapa elimu wakulima na viongozi wa AMCOS namna ya kutumia Mfumo huo.

“Anzeni kutoa mafunzo ili lisije kuwa ni jambo la kushtukiza kwa wakulima ili wawe na uelewa nini kinaenda kufanyika na Mimi na Naibu wangu tutafanya ziara katika maeneo hayo kufuatilia mwenendo wa haya ninayoyaagiza,” amesema Mhe. Bashe.

Aidha, Mhe. Waziri ameelekeza ‘*bidding’* kwa wafanyabiashara zitafanywa 'online' kila siku baada ya makusanyo ya Pamba kwa masaa nane hadi tisa mchana bei ya juu itakayopatikana kwenye kila kituo cha mauzo ndio wakulima wanakuwa wameuza na kupatiwa fedha zao.

“Mkulima akipima mzigo wake apewe risiti ya kukabidhi mzigo ghalani tu na baada ya mnada kukamilika basi mkulima awe ameuza Pamba yake kwa gharama iliyopatikana. Hivyo, mnada uwe kuanzia saa 2 mpaka saa 9 mchana halafu ndiyo taratibu za mauzo ziendelee na mkulima apokee ujumbe wa mauzo yake kupitia simu yake,” amesema Mhe. Bashe.

Akizungumza katika kikao hicho Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, amesema Mfumo huu utamrahisishia mkulima kuuza Pamba yake kwa urahisi na uharaka na mnunuzi atakuwa amepunguza gharama za kusafiri kwenda vituo vya ununuzi na ataweza kufanya *'bidding'* popote alipo.

Dkt. Ndiege amesema ili kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi, amezitaka Bodi ya Stakabadhi za Ghala, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi ya Pamba kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuendelea kuboresha Mfumo wa mauzo ya mazao kwa lengo la kumsaidia mkulima aweze kunufaika na mazao anayozalisha.

“Nichukue nafasi hii kuwapongeza wataalamu mliyofanya kazi hii na kuwashukuru kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kuandaa Mfumo huu ambao una lengo la kumsaidia mkulima; tuendelee kushirikiana ili wakulima waweze kupata huduma iliyo bora zaidi,” amesema Dkt. Ndiege.

## WAKULIMA WA TUMBAKU WALIME NA MAZAO MENGINE - WAZIRI BASHE




*Waziri wa Kilimo Mhe.Hussein Bashe akiwa katika picha ya pamoja na wadau wa Zao la Tumbaku katika Semina ya Sheria na Sera mbalimbali za Sekta ya Tumbaku iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 03 Februari, 2023*

Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe, amewataka wadau wa zao la Tumbaku nchini kuwahamasisha wakulima wa zao hilo kulima mazao mengine kwenye maeneo yao badala ya kutegemea Tumbaku peke yake.

Waziri Bashe amesema hayo Februari 3, 2023 Jijini Dodoma kwenye semina ya Sheria na Sera mbalimbali za Sekta ya Tumbaku iliyoshirikisha kampuni za ununuzi wa zao hilo, wakulima na wadau wengine. Waziri Bashe amesema, kwa wakulima wa tumbaku kulima mazao mchanganyiko itawawezesha kunufaika zaidi kwani watakuwa wanapata mapato kutoka katika mazao tofauti tofauti.

“Wakulima hawa wa tumbaku ni lazima kuendelea kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kulima mazao mchanganyiko kwa kuwa hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwawezesha kunufaika zaidi na kilimo kwa kuwa watakuwa na wigo mpana wa mazao ya kuuza,” Waziri Bashe alisisitiza.

Ameongeza kuwa, iwapo ikitokea mkulima kapata tatizo lolote kwenye zao la Tumbaku anakuwa kwenye mazingira mazuri zaidi ya kupata kipato kwenye mazao mengine

kwasababu anakuwa hategemei zao moja. Amesema kuwa, Serikali itaendelea kupigania haki za wakulima nchini wakiwemo wakulima wa Tumbaku ambapo amefafanua kuwa Wizara inazidi kujipanga katika kuhakikisha kuwa kilimo cha Tumbaku kinakuwa na tija kwa uchumi wa nchi na wakulima kwa ujumla.

Amesema kuwa katika kuhakikisha azma hiyo inatimia wizara imekuwa ikilinda maslahi yao hasa kwa kuwataka wafanyabiashara wanaotaka kuingiza Tumbaku kutoka nje ya nchi kuja kuwekeza kwenye zao hilo hapa nchini ili kuliongezea tija na kuliwezesha kuchangia kwenye pato la Taifa.




*Waziri wa Kilimo Mhe.Hussein Bashe akizungumza na wadau wa Zao la Tumbaku katika Semina ya Sheria na Sera mbalimbali za Sekta ya Tumbaku iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 03 Februari, 2023*

“Mimi kipaumbele changu kimekuwa ni kuwasaidia wakulima na tena kuwawezesha wakulima kunufaika na kilimo na nitahakikisha kuwa wakulima wanazidi kunufaika. Kumekuwa na mtazamo kuwa kilimo ni bidhaa ya jamii yani asiyelima amekuwa ni kama analima tutaubadili mtazamo huu,” Waziri Bashe alisisitiza.

“Katika kuhakikisha mkulima anazidi kunufaika Wizara itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha anapata faida na ifahamike kuwa tutaongeza uzalishaji ili kudhibiti mfumuko wa bei lakini siyo kwa kufunga mipaka,” amesema Mhe. Bashe.

## MFUMO WA MUVU UTARAHISISHA UTOAJI HUDUMA KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA

Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara Frank Kanyusi, amesema kuwa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa kielekroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) utarahisisha utoaji huduma katika Vyama vya Ushirika kwa wananchi.



*Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara ambaye ni Mwanasheria Sekretarieti ya Mkuu wa Mkoa akimkabidhi Kompyuta Mpakato Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Mtwara Ibrahim Kakozi wakati wa Mafunzo ya MUVU yaliyofanyika Mkoani Mtwara tarehe 11 Januari, 2023.*

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu kuhusu matumizi ya Mfumo huo yaliyoanza tarehe 11/01/2023,Kanyusi amesema kuwa TEHAMA ni njia rahisi inayowawezesha watendaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Wanaushirika kwa ujumla kupata taarifa mbalimbali katika utendaji wa kazi pamoja na kupata taarifa za wakulima walioko kwenye vyama vya Ushirika.

Washiriki wa mafunzo haya ni Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa mikoa, Maafisa Ushirika, Mameneja na Wenyeviti wa vyama Vikuu vya Ushirika kutoka mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara.
"Mfumo huu utakwenda kutoa fursa kwa Tume, Vyama vya Ushirika pamoja na wadau wake kuwasiliana pamoja na kutekeleza majukumu yake kupitia mfumo huu; hivyo niwaombe washiriki wa mafunzo haya kuzingatia yale yanayoelekezwa ili kuweza kwenda kutekeleza kazi kwa ufanisi zaidi.

Naye Mwakilishi wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Valency Karunde ambaye ni Mhasibu Mkuu waTCDC amesema kuwa mfumo huu utapunguza ubadhilifu katika Vyama vya Ushirika.

"Bila taarifa inamaana hata udhibiti wa shughuli za Vyama vya Ushirika unakuwa ni mgumu, hivyo kupitia Mfumo huu ni rahisi kupata upatikanaji wa taarifa kupitia kwenye vyama vya Ushirika," amesema Karunde.

Aidha Karunde amesema kuwa Mfumo huu utapunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Ushirika; ambapo wakulima wa vijijini hawatahitajika kusafiri kwenda katika ofisi za Wilaya au Mkoa kupata taarifa juu ya ununuzi na uuzaji wa mazao, badala yake watazipata kupitia mfumo huu.

Mwenyekiti wa TANECU LTD Karimu Kipole, ambaye ni mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo ameishukuru Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kutoa mafunzo kuhusu Mfumo ambayo yatawasaidia kufanya kazi kwa urahisi na kwa ufasaha zaidi na kuweka uwazi katika utendaji kazi.

"Kupitia mafunzo haya tunaamini kuwa kila kitu tutakachokwenda kukifanya kitakuwa bayana, pia mfumo huu utasaidia sana kuondoa watendaji wabadhilifu," amesema kipole. Ameongeza kuwa viongozi wa Vyama vya Ushirika watahakikisha mafunzo haya yanawafikia Watendaji wa Vyama vya Ushirika katika ngazi zote.

Mafunzo haya ya Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika tayari yamefanyika kwa mikoa ishirini na sita ya Tanzania Bara ambapo washiriki wa mafunzo haya ni Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa mikoa, Maafisa Ushirika, Mameneja na Wenyeviti wa vyama Vikuu vya Ushirika.

## MFUMO WA KUSAJILI WAKULIMA WA PAMBA KIDIGITALI WAANZISHWA



*Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe akizungumza na wataalam wa "Mkulima Hub" akiwa ofisini kwake Jijini Dodoma tarehe 07 Februari, 2023*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kushirikisha na Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB), Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) wameanzisha Mfumo wa kusajili wakulima ujulikanao kama "Mkulima Hub".

Mfumo huo unatumika kwa kuanza kusajili wakulima wa Pamba kwa njia ya kidigitali ambapo utamsaidia Mkulima katika shughuli zote za kilimo ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa pembejeo za kilimo, mavuno, na wakati wa uuzaji wa mazao yake.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe amekutana na Taasisi husika Februari 7, 2023 Jijini Dodoma na kuridhia kuanza kutumika kwa Mfumo huo ili kumsaidia Mkulima.

## TCDC IMEDHAMIRIA KUBORESHA MFUMO WA USHIRIKA – NSEKELA

Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Abdumajid Nsekela, amesema TCDC imedhamiria kuboresha mfumo wa Ushirika na kuwa wa kibiashara na kisasa zaidi. Amesema lengo ni kuongeza ushiriki wa wananchi katika sekta mbalimbali na kuongeza mchango wa Ushirika katika kupambana na umasikini pamoja na kukuza uchumi wa nchi.




*Mwenyekiti waTume ya Maendeleo ya Ushirika (katikati) akiwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya TCDC Irene Madeje (kushoto) pamoja na Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC Dkt.Benson Ndiege (kulia kwake) na Wadau na watendaji wa Ushirika katika kikao cha wadau wa Ushirika kilichofanyika tarehe 02 Februari,2023, Jijini Dar es salaam.*

Nsekela amesema hayo tarehe Februari 02, 2023 wakati wa Mkutano na Waandishi wa Habari Jijini Dar es Salam. Pia Mwenyekiti amesema Kamisheni inaweka nguvu katika uanzishwaji wa Mfumo wa kidijitali ili kuongeza ufanisi wa Vyama vya Ushirika na kuimarisha taasisi zinazohusika na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

"Tutaendelea kutoa elimu juu ya dhana ya Ushirika ili kuongeza ushiriki wa sekta mbalimbali, na kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika," amesema Nsekela. Aidha, Mwenyekiti wa Tume Nsekela amesema TCDC kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) wameandaa Mkutano maalumu wa Wadau wa Sekta ya Ushirika unaotarajiwa kufanyika Februari 27, 2023.

Kwa Upande wake Mrajis wa Vyama vya Ushirika Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt Benson Ndiege, amesema Sekta ya Ushirika imeboreshwa na kuongeza wigo wa Ushirika katika sekta mbalimbali na pia kuongezeka kwa mitaji katika vyama na kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya Serikali hususani katika sekta ya Kilimo ambapo tozo za mazao 12 zinakusanywa kupitia Ushirika.

Dkt. ndiege amesema kuwa katika mwaka 2021/2022 Serikali ilipokea jumla ya Shilingi 15,144,077,319.16 zikiwa ni fedha za ushuru unaotokana na zao la Korosho uliolipwa na Vyama vya TANECU, MAMCU, RUNALI, LINDI MWAMBAO, TAMCU NA CORECU na shilingi 1,041,957,051.00 zimepokelewa na Mamlaka za Serikali kama ushuru kutoka katika Vyama vya Ushirika KDCU NA KCU akupitia zao la Kahawa.

## VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO VYATAKIWA KUFANYA UWEKEZAJI NA KUTUMIA TEHAMA



*Naibu Mrajis wa Vyama Vya Ushirika (Udhibiti na Usimamizi) Collins Nyakunga akimkabidhi cheti cha Ushiriki wa Mafunzo kwa Mkurugenzi wa WAKANDI GROUP Stain Andreasen wakati wa Jukwaa la Viongozi wa SACCOS lililofanyika Jijini Dodoma tarehe 21 Februari, 2023*

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika - Udhibiti, Collins Nyakunga, amewataka Viongozi wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kufanya Uwekezaji na matumizi bora ya TEHAMA, na kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali.

Akiongea kwenye Jukwaa la Viongozi wa SACCOS lililofunguliwa tarehe Februari 21, 2023 Mjini Korogwe Mkoani Tanga, amewataka Viongozi hao kufanya ubunifu unaoendana na mahitaji ya soko la fedha pamoja na kuzingatia mabadiliko yaliyopo kwenye Sekta ya Fedha pamoja na mahitaji ya wanachama.

"Simamieni vyema rasilimali za vyama vyetu ikiwemo kuhakikisha tunapunguza migogoro na malalamiko ya wanachama," amesema Naibu Mrajis.

## WATENDAJI WA USHIRIKA WATAKIWA KUFUATA TARATIBU NA SHERIA ZA USHIRIKA



*Kaimu Naibu Mrajis (Uratibu na Uhamasishaji) wa Vyama vya Ushirika, Consolata Kiluma akizungumza na Watendaji wa Ushirika katika jukwaa la Ushirika Mkoani Pwani tarehe 22 Februari, 2023*

Kaimu Naibu Mrajis (Uratibu na Uhamasishaji) wa Vyama vya Ushirika, Consolata Kiluma amevitaka Vyama vya Ushirika vya mkoa wa Pwani kufuata taratibu na Sheria za Ushirika ili kuufanya Ushirika kuwa wenye nguvu zaidi.

Naibu Mrajis ameyasema hayo Februari 22,2023 mkoani Pwani katika Jukwaa la Ushirika lenye lengo la kufanya tathmini ya shughuli za Vyama vya Ushirika kila mwaka.

Aidha, Naibu Mrajis amevitaka Vyama vya Ushirika kuutangaza Ushirika ili watu waelewe mafanikio na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Ushirika.

"Nitoe wito kwenu watendaji wa Ushirika kuutangaza ushirika kupitia vyombo mbalimbali vya Habari zikiwemo Televisheni, Redio, Magazeti, na Mitandao ya Kijamii ili utambulike na wanaushirika, wananchi na Taifa kwa ujumla," amesema.

Naye Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Pwani, Abdillah Mutabazi, amesema kuwa atahakikisha wanausimamia Ushirika kwa kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa na Ushirika ili kuwajengea wanaushirika na wasio wanaushirika kuwa na Imani na Ushirika.

Kwa upande wa Mkaguzi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Pwani na Dar es salaam Brighton Mwang'onda amesema kuwa ili kuondokana na Hati Chafu, watendaji wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanakuwa na taarifa sahihi za kifedha.

# MPANGO WA KUBORESHA VYAMA VYA USHIRIKA WAJADILIWA



*Mwenyekiti wa Kamisheni (TCDC), Abdulmajid Nsekela akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa Ushirika uliofanyika tarehe 27 Februari, 2023 Jijini Dar es Salaam*

Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imeanza kutekeleza mpango wa kubadili namna ya kuendesha Vyama vya Ushirika na kuviwezesha kutumia Teknolojia za kisasa katika kufanya shughuli zao.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Abdulmajid Nsekela, ametoa taarifa hiyo tarehe Februari 27, 2023 wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Wadau wa Ushirika Jijini Dar es Salaam, unaolenga kujadili maendeleo ya Ushirika na kuweka mkakati wa kuimarisha Sekta hiyo hapa Nchini.

Nsekela amesema, Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidijitali utaongeza ufanisi wa kiutendaji katika Vyama vya Ushirika, pamoja na Mamlaka za Usimamizi wa Sekta hiyo. Ameongeza kuwa, pamoja na mambo mengine, mapendekezo yatakayotolewa katika mkutano huo yatasaidia kuboresha Mfumo wa Ushirika na kuufanya wa kisasa zaidi na kuwawezesha wananchi kushiriki ipasavyo kwa ustawi wao na wa Taifa kwa ujumla.

“Ni matumaini yangu kuwa Maazimio yatakayofikiwa kupitia mkutano huu yatapaswa kutekelezwa ipasavyo na kila mdau na kwamba taarifa ya utekelezaji itakuwa inatolewa na kujadiliwa mara kwa mara,”amesema Nsekela.

Kwa upande wake Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, amesema lengo kubwa la mkutano huo wa Wadau wa Ushirika ni kujadili maendeleo ya Ushirika na kuweka Mkakati wa kuimarisha Sekta hiyo hapa nchini.

“Mkutano huu ni muhimu kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo ya Ushirika hapa nchini, lakini pia tumekutana wadau wote ili kuja na mapendekezo ya pamoja ya kuendeleza Sekta hii kwa Maendeleo ya Taifa,” ameongeza Mrajis.

Aidha, Dkt. Ndiege amesema, kila aliyepewa dhamana atekeleze majukumu yake ili kuujenga Ushirika ulio imara ambao utawasaidia wananchi katika kuboresha uchumi wao.

“Tushirikiane kuujenga Ushirika nafurahi sasa hivi kuona Vyama Vikuu vya Ushirika vinasaidia katika kutoa misaada katika huduma za kijamii, endeleeni kurudisha mnachokipata kwa jamii,” amesema Dkt. Ndiege.

# VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA WATAKIWA KUONDOKANANA HATI CHAFU



*Kaimu Naibu Mrajis (Uratibu na Uhamasishaji) Consolata Kiluma akimkabidhi tuzo ya Utendaji bora Mwenyekiti wa UDIDA SACCOS Jasson Rutatinisibwa katika Jukwaa la Ushirika lililofanyika Mkoani Shinyanga tarehe 06 Machi, 2023*

Kaimu Naibu Mrajis (Uratibu na Uhamasishaji) wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Consolata Kiluma, amewataka Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika mkoani Shinyanga kuondokana na Hati Chafu ili kuwa na Ushirika wenye tija.

Wito huo umetolewa Machi 06, 2023 katika Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika mkoani Shinyanga lenye lengo la kujadili changamoto, mafanikio na maazimio ya Ushirika kwa ujumla.

"Nitoe wito kwa watendaji wa Ushirika kuondokana na Hati Chafu, tujadiliane na tusaidiane kama Wanaushirika, namna gani tutafanya kuweza kuepukana na changamoto zinazoweza kujitokeza kuhusiana na Hati Chafu," amesema Kiluma.

Aidha, Kaimu Naibu Mrajis amewataka wanaushirika kuendelea kuchangia Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL) ili kuweza kukamilisha uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ambayo ni mkombozi mkubwa kwa Wanaushirika kwa ujumla.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa wa Shinyanga Mabala Mlolwa amewataka Viongozi wa Vyama Vya Ushirika kuwa mfano kwa Vyama wanavyoviongoza.

"Unapopewa dhamana ya Uongozi unatakiwa kuwa mfano kwa wakulima, kiongozi unatakiwa kuwa na Shamba la mfano ili kuweza kusimamia wakulima. Huwezi kujadili changamoto za Wakulima wakati huna shamba, usipofanya hivyo itakuwa ni vigumu kujua changamoto wanazozipitia Wakulima," amesema Mlolwa.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Mhe. Emmanuel Cherehani, ambaye pia ni mwanaushirika amesema kuwa ili kuweza kuwa na Hati Safi yawapasa viongozi kusimamia watendaji wa Vyama vya Ushirika kuandika vitabu, kufunga Hesabu ili kusaidia kuwa na namna bora ya matumizi bora ya Fedha.

"Ushirika kwa Sasa unafanya vizuri, Viongozi wasaidieni Vijana kuandika vitabu na kufunga mahesabu ili kuondokana na Hati Chafu," amesema Mhe. Cherehani.

Katika katika jukwaa hilo pia, Ofisi ya Mrajis mkoa wa Shinyanga imetoa Tuzo mbalimbali kwa Vyama vya Ushirika vilivyofanya vizuri katika utendaji kazi kwa kuwa wabunifu, uwezo na utoaji wa huduma bora kwa wakulima.Vyama vilivyopata tuzo hizo ni UDIDA SACCOS, IPANDIKILO SACCOS, Chama Kikuu cha Ushirika - KACU, NGOKOLO AMCOS, Shinyanga Municipal SACCOS na Biashara SACCOS.

Akiongea mara baada ya utowaji wa tuzo hizo, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Shinyanga, Hilda Boniphace, amevitaka Vyama kuendelea kufanya vizuri kwa kufuata taratibu na Sheria za Vyama vya Ushirika.

## VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO VYATAKIWA KUJITANGAZA

SCCULT




*Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, (Usimamizi na Udhibiti), Collins Nyakunga (aliyekaa watatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mameneja wa SACCOS mbalimbali Nchini katika kikao cha nne cha Vingozi hao kilichofanyika Jijini Dodoma tarehe 14 Machi 2023*

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika - Usimamizi na Udhibiti, Collins Nyakunga, amevitaka Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) kutumia Vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii kujitangaza.

Nyakunga amesema, vyama hivyo vinafanya mambo mengi mazuri ambayo yanapaswa kufahamika kwa jamii na kueleza ni vyema vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusika katika kuvitangaza.

Nyakunga ametoa kauli hiyo Machi 14,2023 wakati wa ufunguzi wa Kikao cha Nne cha Mameneja wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo kinachofanyika kwa siku nne Jijini Dodoma.

Kauli mbiu ya Mkutano huo ni “Meneja Wajibika, Timiza wajibu wako Ongeza thamani kwa Huduma Bora”. Kauli mbiu iliyolenga kuongeza ari ya watoa huduma kwa wateja.

Naibu Mrajis Nyakunga amesema Ushirika ni sehemu sahihi ambayo mtu yeyote

anapokuwepo anakuwa na uhakika kuwa wapo mahala salama patakapowafanya kunyanyuka kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja au kikundi.

Vilevile Nyakunga amehimiza uanzishwaji Benki ya Taifa ya Ushirika na amesema Benki ya Ushirika ikianzishwa itafikisha mbali Ushirika hivyo ni wajibu wa wana SACCOS kuendelea kununua Hisa ambazo zitafanikisha benki hiyo kupata mtaji wa kuendesha na kuifanya kuwa ni benki ya Ushirika.

Amesema Nyakunga zipo SACCOS zenye mitaji mikubwa ambayo tunafikiri waanze kukopesha Vyama Vikuu '*UNION'* ambazo fedha zao ni za msimu, tutakaa vikao na kujadiliana hili na kufikia makubaliano, ili hata '*UNION'* ambazo wanapata fedha kwa msimu wanunue hisa katika benki hiyo.

“UNION zikikopeshwa na SACCOS tunatarajia baada ya misimu miwili wawe wamemaliza deni ili kuwezesha UNION zingine kukopeshwa.

"Tutakuwa makini sana katika kusimamia ulipaji wa deni hilo hivyo wakopeshwaji wanapaswa kutambua ukikopa lazima ulipe na ulipe kwa wakati mliokubaliana,” Nyakunga alisisitiza.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji SCULLT (1992) Ltd, Hassan Mnyone ameeleza kuwa, kila Meneja anapaswa kuwa mbunifu katika kazi zake ili aweze kuendesha SACCOS yake na kuifanya izidi kukua na kuwa imara kila siku na kueleza siku ya jana ya Meneja haipaswi kufanana na ya leo.

Aidha, amesema ili kupata matokeo chanya katika vyama ni wajibu wa Meneja kufanya kazi kwa kujituma na kusimamia SACCOS kwa kufuata sheria, taratibuna kanuni ziendele kuwa hai.

Vile vile amewaasa Mameneja hao kufanya kazi kwa maslahi ya wanachama na si kujiangalia wenyewe kwani Nguzo ya chama ni wanachama hivyo wajitahidi kupokea marekebisho na maoni yanayotoka kwa wanachama kwa lengo la kujenga Vyama.

## SIMCU FUFUENI VIWANDA VYENU - RC SIMIYU




*Mkuu wa mkoa wa Simiyu, Mheshimiwa Dkt.Yahaya Nawanda akizungumza wakati wa Mkutano Mkuu wa Sita wa Chama Kikuu cha Ushirika (SIMCU) Mkoani Simiyu tarehe 17 Machi, 2023*

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mheshimiwa Dkt.Yahaya Nawanda, ametoa Rai kwa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Simiyu SIMCU (2018) Ltd kufufua Viwanda vyao na kuanza kufanya kazi ili kuimarisha Mnyororo wa thamani wa zao la Pamba.

Dkt Nawanda amesema SIMCU (2018) Ltd wanatakiwa kukifanya kilimo cha Pamba kuwa chenye tija na thamani kwa wakulima na jamii kwa ujumla kwani MheDkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewezakuongeza bei ya pamba kutoka Shilingi 1,200 msimu 2021/22 hadi Shilingi 2,050 msimu huu 2022/23.

Dkt. Nawanda ametoa rai hiyo alipokua akihutubia wakati wa Mkutano Mkuu wa Sita wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Simiyu SIMCU (2018) Ltd akiwa ni Mgeni Rasmi katika mkutano huo uliofanyika Machi 17, 2023 Mkoani Simiyu.

Aidha, Dkt. Nawanda amesema Mkoa wa Simiyu ni mkoa pekee unaolima Pamba Hai "Organic Cotton" na kuwataka wananchi kufahamu uzuri wa pamba hiyo na hilo ni jukumu la viongozi wa Ushirika Mkoani Simiyu kuitangaza Pamba hiyo ya kipekee.

Vilevile, Dkt. Nawanda amewataka Viongozi wa SIMCU (2018) Ltd kuhakikisha wanashiriki na kusimamia kikamilifu zoezi la usambazaji wa viwatilifu na vinyunyizi vya zao la pamba kwa wakulima ambalo linategemea kuanza.

."Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaratibu na kusimamia shughuli ya usambazaji na ugawaji wa dawa hizo kupitia Vyama vya Msingi ambavyo ni wanachama wa SIMCU (2018) Ltd, hatutegemei kusikia malalamiko kwa wakulima wetu na mtambue kabisa yoyote atakayeenda kinyume na maelekezo ya Serikali atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria," Dkt Nawanda aliongeza.

Mgeni Rasmi Dkt. Nawanda amesema Serikali imekusudia msimu 2023/2024 kuanza kutumia mfumo wa kidigitali katika upimaji na uuzaji wa zao la Pamba. Hivyo, Viongozi wa Ushirikia wanapaswa kuanza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mifumo inavyotumika kuuza mazao ya wakulima ili kuwajengea wakulima uelewa kabla ya kuanza utekelezaji.

Kwa upande wake Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika - Uratibu na Uhamasishaji, Consolata Kiluma amesema kuwa ili kuwe na Vyama vya Ushirika imara na vinavyojitegemea kiuchumi na kutoa huduma stahiki kwa wanachama inapaswa Vyama vya Ushirika kujenga mitaji kwa kuwekeza katika Benki ya Ushirika ya Kitaifa inayotarajia kuanza hivi karibuni.

Aidha, Consolata alisisitiza kuwa huu ni wakati wa SIMCU na AMCOS kuondokana na hati zenye mashaka za ukaguzi kwa kufanya mambo yote kwa kufuata utaratibu na maelekezo na ushauri unaotolewa na COASCO ili Vyama hivyo visiingie tena katika kundi la hati zenye mashaka.

Vilevile Naibu Mrajis alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha Viongozi wote wa Ushirika kuwa wapo kwa mujibu wa Sheria hivyo wanapaswa kusimamia na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake na Masharti ya Vyama hivyo na Sheria nyingine za nchi.

## TANZANIA YAWAHAKIKISHIA WAFANYABIASHARA WA SUDAN YAKUSINI UPATIKANAJI WA MAZAO YA




*Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt Benson Ndiege akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Taasisi za Kiserikali na Sekta Binafsi kwenye Mkutano wa Fursa za Kibiashara na Masoko Nchini Sudani Kusini tarehe 22 Machi, 2023*

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, 2023 ameshiriki Mkutano wa Fursa za Kibiashara na Masoko nchini Sudan ya Kusini ambapo amewahakikishia Wafanyabiashara wa nchi hiyo upatikanaji kwa wingi wa mazao bora ya kilimo kutoka Tanzania kupitia Vyama vya Ushirika na Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Mkutano huo umeandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Sudani ya Kusini, kwa lengo la kujadili na kuunganisha fursa za biashara na masoko ya mazao baina ya nchi hizi mbili, umefanyika kwa siku mbili kuanzia tarehe 22 - 23 Machi, 2023.

Katika mkutano huo, Mrajis amepata fursa ya kuwasilisha na kueleza fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye Sekta ya Kilimo kupitia Vyama vya Ushirika. Baadhi ya maeneo yaliyoelezwa ni pamoja na uwepo wa fursa za masoko ya mazao na bidhaa zinazozalishwa na kuuzwa kupitia Vyama vya Ushirika, upatikanaji wa pembejeo za kilimo kupitia Vyama vya Ushirika, pamoja na uwekezaji katika Vyama vya Ushirika.

Aidha, Mwakilishi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Erick Temu, wameeleza namna Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unavyofanya kazi na kutoa fursa kwa wafanyabiashara kupata mazao yenye ubora kupitia Vyama vya Ushirika.

Mkutano huo unafanyika Mjini Juba na unahudhuriwa na Wakuu wa Taasisi za Serikali pamoja na Sekta Binafsi kutoka Tanzania.

Taasisi za Serikali zinazoshiriki ni pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Hospitali yaTaifa ya Muhimbili, Shirika la Bima la Taifa (NIC), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Taasisi zingine zilizoshiriki Mkutano huo ni pamoja na Tume ya Ushindani Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Shirika la Ndege Tanzania (ATC), Mamlaka ya Usimamizi wa Petroli Tanzania (PURA), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Kwa upande wa Sekta Binafsi, makampuni yanaoshiriki mkutano huo ni Kampuni ya Tobage, Junaco na Kusa Investment na SUMA JKT.

## MPANGO WA BAJETI NA VIPAUMBELE KWA MWAKA 2023/2024 VYA TCDC VYAJADILIWA



*Kaimu Mwenyekiti Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Gabriel Mwita, akizungumza katika kikao cha kupitia na kujadili Mpango wa Bajeti ya Tume kwa Mwaka 2023/2024 Baraza lililofanyika tarehe 24 Machi, 2023 Jijini Dodoma*

Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) limepitia na kujadili Mpango wa Bajeti ya Tume kwa Mwaka 2023/2024.Bajeti hiyo inategemea kutumika katika ya Matumizi ya kawaida ya Tume kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Miradi ya Maendeleo.

Mpango huo wa Bajeti wa Tume umepitishwa Machi 24, 2023 wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika TCDC lililofanyika Jijini Dodoma.

Kaimu Mwenyekiti Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Gabriel Mwita, amewataka wajumbe wa Baraza hilo kurudisha mr`ejesho wa yale

yaliyojadiliwa katika kikao hicho kwa kuwa wao ndiyo wajumbe wanaowawakilisha watumishi wengine wa TCDC.

Aidha, Mwita aliwashukuru Wajumbe kwa kufika katika kikao na kuweza kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya bajeti hiyo ambayo ndiyo muhimili katika Utekelezaji wa Majukumu ya TCDC.

## MAFANIKIO YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MKOA WA LINDI

Mkoa wa Lindi una jumla ya Vyama ya Ushirika vya Msingi 195, (SACCOS 17, AMCOS 165, na vyama vingine 13) na vyama Vikuu vya Ushirika viwili ambavyo ni Chama Kikuu cha LINDI MWAMBAO kinachohudumia Halmashauri ya Kilwa, Mtama na Lindi Manispaa, na Chama kikuu cha Ushirika cha RUNALI kinachohudumia Halmashauri za Ruangwa, Nachingwea pamoja na Liwale.

Mkoa wa Lindi una jumla ya Halmashauri 6; Halmashauri ya Lindi Manispaa, Halmashauri ya Lindi, Kilwa, Nachingwea, Ruangwa na Liwale na Halmashauri za Wilaya 5). Idadi ya wanachama katika mkoa ni 46,291, kati ya hao wanaume ni 23,035 na wanawake ni 23,256.

Mazao ya Kimkakati yanayolimwa katika Mkoa huu ni Korosho na Ufuta ambayo yote huuzwa kwenye Ushirika kwa kutumia mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Mkoa wa Lindi kupitia sekta ya Ushirika imeweza kupata mafanikio yafuatayo: Asilimia 88.3 ya vyama vyote vya mkoa

wa Lindi vinajishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwa sambamba na malengo ya uanzishwaji wake. Vyama vya Ushirika vya msingi vya mazao vimeendelea kukusanya na kuuza mazao ya wakulima na wanachama wao katika mazao ya Ufuta na Korosho kupitia mfumo wa Stakabadhi ya mazao Ghalani.




*Kituo cha Malipo kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika RUNALI kilichopo katika Halmashauri ya Liwale mkoani Lindi*

**Mkoa umeweza** kusimamia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa kuwaunganisha wadau wote wanaohusika na kusimamia kikamilifu malipo ya mazao ya wakulima walio wanachama na wasio wanachama na kusababisha utulivu wa kiuchumi kwa wanachama na wakulima waliokusanya mazao yao kwenye Vyama vya Msingi.



*Kituo cha Malipo kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika RUNALI kilichopo katika Halmashauri ya Nachingwea mkoani Lindi.*

### Ukusanyaji wa Tozo

Mkoa wa Lindi umesimamia na kurahisisha ukusanyaji wa tozo zote za serikali na wadau mbalimbali, katika msimu wa korosho 2022/2023.Jumla ya kilo 57,063,660 ziliuzwa na Vyama vya Ushirika kupitia Mfumo wa stakabadhi za ghala na katika kiasi hicho tozo zilizokusanywa ni pamoja na ushuru wa Halmashauri zote sita kiasi cha Tshs 3,249,204,800.40.Tozo ya Mrajis wa vyama vya Ushirika kiasi cha Tshs 228,254,640/=.

Aidha mfuko wa Elimu wa Halmashauri ulikusanya kiasi cha Tshs 1,483,655,160, Mfuko wa Elimu Mkoa Tshs 114,127,320, Tozo ya TARI 1,426,591,500, Tozo ya Bodi ya Korosho Tshs 1,426,591,500, Ugani na Payment Center Tshs 114,127,320, Ushuru wa Unioni Tshs 1,997,228,100 pamoja na Ushuru wa vyama vya msingi Tshs 3,709,137,900. Yote haya yamewezekana kutokana na usimamizi thabiti uliowekwa kwenye vyama vya Ushirika kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini.

**Ujenzi wa Maghala**

Aidha Vyama vya Ushirika mkoani Lindi vimewezesha Ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao ya wakulima ni moja ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2022/2023, maghaha 6 na nyumba za kulala wageni 2 zimejengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Halmashauri ya Ruagwa maghala 12, Halmashauri ya Mtama maghala 3, Lindi manispaa maghala 2, na Halmashauri zilizobaki vyama vya msingi vinamiliki maghala yao waliyoyajenga kabla ya Mwaka 2022/2023, Hii imepelekea uhifadhi bora wa mazao ya wakulima na kufanya ongezeko la bei ya mazao yako yanapofika mnadani.



*Ghala dogo la kuhifadhia Pembejeo na Vifungashio*

**Upatikanaji wa Mikopo na Pembejeo**

Mkoa wa Lindi umeweza kuviunganisha Vyama na Taasisi za fedha ili kuweza kupata mikopo ya pembejeo kwa ajili ya wakulima wanachama wao, mikopo ya ujenzi wa maghala na mikopo ya ununuzi wa vyombo vya usafiri kwa baadhi ya vyama vya msingi.

**Vilevile V**yama Vikuu vimeendelea kutekeleza miradi mikubwa mfano mzuri ni Chama Kikuu cha RUNALI wamekamilisha ujenzi wa ghala kubwa lenye uwezo wa kuchukua Tani 10,000 za mazao, vituo vya malipo ya fedha za wakulima katika Halmashauri zote tatu za Ruangwa Nachingwea na Liwale pamoja na ghala dogo la kuhifadhia pembejeo na vifungashio, kwa upande wa Lindi mwambao wapo kwenye utekelezaji wa ujenzi wa

ofisi ya chama ambayo ipo hatua za mwisho pamoja na ujenzi wa ghala ambao upo katika hatua za mwanzo.

**Usimamizi wa Vyama vya Ushirika**

Tume ya Maendeleo ya ushirika kupitia ofisi ya Mrajis Msaidizi mkoa wa Lindi imeendelea kuvisimamia vyama na kuvipatia miongozo mbalimbali ya kurahisisha utendaji kazi katika kuleta ufanisi na kupunguza malalamiko na migogoro kwenye vyama na wanachama wao na wadau wengine.

## WATUMISHI WA TCDC WAPIGWA MSASA MAAMBUKIZI YA VVU/UKIMWI NA MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZA

## KILIMO KUPITIA VYAMA VYAUSHIRIKA



*Naibu Mrajis wa Vyama Vya Ushirika, (Udhibiti na Usimamizi) Collins Nyakunga akizungumza wakati wa Ufunguzi wa Mafunzo kuhusu Maambukizi ya VVU/UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza kwa Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika yaliyotolewa Jijini Dodoma tarehe 05 April, 2023.*

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga, ametoa wito kwa Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kuzingatia Kanuni za Afya kwa lengo la kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI pamoja na magonjwa yasiyoambukiza ili kutunza nguvu kazi pamoja na ustawi wa jamii.

Wito huo umetolewa Aprili 05, 2023 wakati wa ufunguzi wa mafunzo kuhusu Maambukizi ya VVU/UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza kwa Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika yaliyotolewa Jijini Dodoma.

Akifungua mafunzo hayo Naibu Mrajis amesema mafunzo hayo ni sehemu ya kuunga

mkono jitihada za Serikali kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa kudhibiti VVU/UKIMWI kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza ufanisi katika Utumishi wa Umma.

Sambamba na Mafunzo hayo watumishi wa Tume wamepata fursa ya kupata elimu ya utunzaji na kanuni bora za afya, ushirikiano mahala pa kazi, pamoja na zoezi la upimaji wa afya lililofanyika kwa lengo la kusaidia watumishi kujua vyema afya zao na kuchukua hatua sahihi.

Mafunzo hayo yameratibiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na kuwezeshwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Mkurugenzi Msaidizi-Anuai za Jamii, Mwanaamani Juma Mtoo, aliyeambatana na Dkt. Ibrahim Haule kutoka TACAIDS.

# MKOA WA SIMIYU WADHAMIRIA KUANZISHA VIWANDA NA KUIMARISHA VYAMA VYA USHIRIKA




*Mkuu wa Mkoa wa SIMIYU, Mhe.Dkt.Yahya Nawanda akimkabidhi cheti kwa Kiongozi wa Chama cha Ushirika kilichofanya vizuri kwa Mwaka 2023*

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. Dkt. Yahya Nawanda, amesema Mkoa wa Simiyu umedhamiria kuanzisha viwanda kwa ajili ya kuongeza ajira na kukuza uchumi wa mkoa na nchi kwa ujumla.

Dkt. Nawanda ameyasema hayo alipokuwa akizindua Jukwaa la tatu la Ushirika Mkoa wa Simiyu tarehe 27 Aprili, 2023 Mjini Bariadi.Dkt. Nawanda amesema viwanda vitakavyoanzishwa vitatumia mali ghafi zitazokuwa zinazapatikana kupitia Vyama vya Ushirika na Wakulima wa Mkoa huo na mikoa ya jirani.

Jukwaa la Ushirika mkoani Simiyu lililozinduliwa na kuhudhuriwa na Makamu Mwenyekiti Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Irene Madeje na Naibu Mrajis - Uhamasishaji Consolata Kiluma, Mrajis Msaidizi Mkoa wa Simiyu, Godfrey Mpepo na Wadau wa Ushirika pamoja na Viongozi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Simiyu linalenga kuweka Mkakati wa Pamoja wa kuimarisha Vyama vya Ushirika mkoani humo.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu amesema mkakati ulioko kwa sasa ni kujenga Viwanda Bariadi DC na Bariadi TC ambavyo viwanda hivyo vitaweza kuzalisha ajira 800 - 900, na katika Wilaya ya Busega kutajengwa kiwanda kikubwa cha Sukari ambacho kitazalisha ajira elfu 20. Dkt. Nawanda amesema Mkoa wa Simiyu unalenga kuongeza uzalishaji wa zao la Pamba kufikia tani laki tatu (300,000) ambapo asilimia 60 ya Pamba Hai Nchini inazalishwa katika mkoa wa Simiyu.

Akizungumza katika uzinduzi wa Jukwaa la Ushirika, Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Irene Madeje amewasisitiza Wanaushirika kutumia ipasavyo Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ili uweze kuwasaidia katika kusimamia mali za Ushirika.

Aidha, Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya Ushirika amevitaka Vyama vya Ushirika kuhama kutoka katika matumizi ya pesa taslimu na kuhamia kwenye kutumia Pesa Mtandao (moneyless) ili kupunguza au kuondoa kabisa ubadhilifu katika masuala ya kifedha.

## ZOEZI LA UGAWAJI MALI NA MADENI KWA AMCOS ZA MIWABONDE LA KILOMBERO LAKAMILIKA



*Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika (Usimamizi na Udhibiti) Collins Nyakunga akizungumza wakati wa zoezi la Ugawaji wa Mali na Madeni za AMCOS za miwa Bonde la Mto Kilombero tarehe 24 Juni, 2023*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Bodi ya Sukari Tanzania (TSB) zimesimamia zoezi la Ugawaji wa Mali na Madeni na usainishwaji Hati za makubaliano kwa AMCOS za Miwa bonde la Kilombero baada ya kupangwa kijiografia.

Zoezi hilo limefanyika tarehe 25/04/2023 Ruaha Kidatu katika Halmashauri ya Kilombero na kukamilika baada kikao kazi kilichofanyika na kubaini kuwepo kwa malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na wadau wa Tasnia ya sukari bonde na Vijiji na kata kwa upande wa Kilombero na Kilosa ili kuona hali halisi ya mpangilio wa mashamba na wakulima wa miwa.

Akiongea wakati wa ufunguzi wa zoezi hilo Naibu Mrajis wa Vyama Vya Ushirika (Usimamizi na Udhibiti) Collins Nyakunga, amesema kuwa, changamoto zilizokuwepo kwa wakulima kwa sasa hazitakuwepo tena kwani maeneo yote yameshapangwa kijiografia na hivyo kuwarahisishia wakulima kuweza kufanya maamuzi kwa pamoja.

"Ndugu zangu jambo lililofanyika ni la msingi sana litaturahisishia sana wakati wa kuvuna, kusafirisha na kuwahudumia wakulima kwa wakati na kutatua changamoto kama za moto katika mashamba ya miwa," amesema Nyakunga.

Naibu Mrajis ameongeza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013 kifungu namba 98, inaamriwa kuwa Vyama vyote vya Ushirika ambavyo havijiwezi na havifanyi vizuri tunavihamasisha na kuunda Vyama vya Ushirika vilivyo imara na kuwa na uwezo wa kuzalisha kwa wingi.

Naye Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa wa Morogoro, Keneth Shemdoe amesema kuwa baada ya zoezi hilo kukamilika Vyama vinaenda kujiendesha kibiashara ambapo kila Chama kitakwenda kusimamia misingi ya kijiografia iliyotumika katika Ugawaji wa Mali za vyama hivyo.

"Mali, fedha na samani zote za Vyama vilivyogawanywa leo zimegawanywa kiusawa kwa asilimia 100 kwa kila Chama kwa kuzingatia kiwango cha hisa zilizokuwepo kwa kila Chama cha Ushirika," amesema Shemdoe.

Zoezi hilo pia litasaidia kuongeza uwazi, kusogeza karibu huduma za uvunaji, kutambua maeneo yaliyo mabondeni na kuwapa kipaumbele katika uvunaji, kupunguza kuvuniwa kwa upendeleo, kukopesheka kirahisi kwenye taasisi za kibenk,kuwezesha zoezi la usajili kwa wakulima, kupunguza ajali za moto, kurahisisha miundo mbinu ya barabara za mashambani.

Zoezi hilo limefanikiwa kupanga Vyama kijiografia kutoka AMCOS 20 hadi 17 ambapo kwa upande wa Wilaya ya Kilombero (K1) ni AMCOS 8 na kwa upande wa Wilaya ya Kilosa (K2) ni AMCOS 9.

# WATUMISHI WA TCDC WANG'ARA KWENYE TUZO ZA WAFANYAKAZI BORA MEI MOSI



*Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Jumanne Sagini akimkabidhi Tuzo ya Wafanyakazi Bora Afisa Sheria wa TCDC Albert Mwombeki katika Sherehe zaMeimosi Jijini Dodoma tarehe 01 Mei, 2023*

Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Jumanne Sagini ametoa tuzo kwa wafanyakazi Bora wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) katika Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani ambayo kwa Mkoa wa Dodoma zimefanyika tarehe 01/05/2023 katika viwanja vya Jamhuri Jijini Dodoma.

Akitoa Tuzo hizo zilizowahusisha pia watumishi wengine wa Serikali na Sekta Binafsi Mhe.Sagini amewataka watumishi na waajiri wafanye kazi kwa bidii ili kuepuka migogoro katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Ndugu wafanyakazi,niwaombe muendelee kufanya kazi kwa bidii,weledi na maarifa mkishirikiana na waajiri na Serikali katika kuhakikisha kila sehemu ya kazi Kuna utulivu na utii wa sheria ili kuondoa migogoro isiyo na tija katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa ufanisi," amesema Mhe.Sagini.

Akiongea kwa niaba ya Wafanyakazi wenzake waliopewa Tuzo hizo Valentino Ngoda ambaye ni Afisa TEHAMA amesema kuwa ubunifu, uchapakazi nidhamu na kujitolea ndiko kulikopelekea kuwa mmoja wa Wafanyakazi Bora wa TCDC.

Miongoni wa watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika waliopata tuzo hizo ni Valentino Ngoda (Afisa TEHAMA), Jeremiah Boniphace (Afisa Ushirika) Delius Bushegu (Katibu Muhtasi) na Albert Mwombeki (Afisa Sheria).

## WAKULIMA 681 WA MAZAO YA BUSTANI WAHAMASISHWA KUANZISHA VYAMA VYA USHIRIKA MKOANI KILIMANJARO



*Wakulima mbalimbali wambogamboga na Matunda kutoka katika Halmashauri ya Moshi Vijijini wakiwa katika zoezi la Uhamasishwaji wa Uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa mazao ya Bustani tarehe 05 Mei, 2023*

Timu ya uhamasishaji kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) imekamilisha uhamasishaji wa uanzishaji wa Vyama vya Ushirika wa mazao ya bustani (horticulture)

ambapo zoezi hilo lilifanyika kuanzia tarehe 24 Aprili hadi Mei 05, 2023 katika Halmashauri ya Wilaya za Moshi Vijijini, Moshi Manispaa na Hai.

Ameeleza Afisa Ushirika kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Ndimolwo Laizer kuwa uhamasishaji huo umekamilika tarehe 05/05/ 2023 ambapo matarajio ya awali ni kuvifikia vikundi 18 vya wakulima wa mazao ya Bustani vyenye jumla ya wakulima 298 Baada ya zoezi kukamilika kwa halmashauri hizo jumla ya vikundi 48 vyenye Jumla ya wakulima 681 vimefikiwa na kupatiwa elimu ya uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya Mazao ya Bustani mkoani humo.

Amesema hayo wakati wa uhitimishaji wa zoezi la utoaji elimu wa dhana ya Ushirika kwa lengo la uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika tarehe 05 Mei,2023 katika Vijiji vya Mkalama kata ya Masama Rundugai na Kata ya Weruweru.

Amesema Ndimolwo Laizer Serikali imedhamiria kuwa kufikia 2030 wakulima wote Nchini wakiwemo wa MAZAO ya BUSTANI watakuwa wanazalisha kibiashara ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agenda 10/30 pamoja na faida mbalimbali zinazopatika kupitia Ushirika.

Kwa upande mwingine Afisa Ushirika Mwajuma Myombo amesema kuwa Ushirika kwa Mazao ya Bustani utasaidia kurahisisha huduma zinazohitajika kwa wakulima ikiwemo huduma za ugani sambamba na kuongeza mapato kwa wakulima na Halmashauri husika.

Aidha, amesema kuwa kwa vikundi vilivyokubali kuanzisha Ushirika na ambavyo vimeanzisha Kamati anzilishi watashirikiana nao kuhakikisha mpaka tarehe zilizopangwa za kukutana tena nyaraka zote muhimu kwa ajili ya usajili wa Chama yatakuwa yameandaliwa.

Vyama vya Ushirika vya mazao ya Bustani 14 vinatarajiwa kuanzisha Mkoani Kilimanjaro na wakati wa utekelezaji wa zoezi la uhamasishaji jumla ya Vyama vya Ushirika sinzia 3 vya mazao ya mchanganyiko ikiwemo mazao ya Bustani vimefikiwa na kuhamasishwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Masharti ya Chama, Sheria ya Vyama vya Ushirika na Miongozo mingine waliyojiwekea ili viweze kujibu hitaji la kuanzisha kwa Vyama hivyo.

Aidha, zoezi litakalofuata ni la uandaaji na upitiaji wa nyaraka za usajili zitakazoandaliwa na Kamati anzilishi na kujadiliwa kupitia Mikutano Mikuu ya Kwanza ili Vyama hivyo tarajiwa viweze kusajiliwa.

## MRAJIS MSAIDIZI MKOA WA LINDI AKABIDHIWA GARI KATIKA JUKWAA LA USHIRIKA



*Mkuu wa Mkoa wa Lindi na Kamishina wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Mhe.Zainab Telack (Kushoto) akikabidhi gari kwa Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Lindi Cecilia Philimini kwenye Jukwaa la Ushirika tarehe 18 Mei, 2023.*

Mkuu wa Mkoa wa Lindi na Kamishina wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Mhe. Zainab Telack amekabidhi gari kwa Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Lindi Cecilia Philimini. Gari Hilo limetolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) limekabidhiwa tarehe 18/05/2023 wakati wa Jukwaa la Ushirika la Mkoa wa Lindi lililofanyika Mjini Lindi likiwa na kauli mbinu "Ushirika ni Biashara". Kwenye jukwaa hilo Mkuu wa Mkoa,ametoa rai kwa wana Lindi wanaojishugulisha na masuala ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji kujiunga na Vyama vya Ushirika ili waweze kuuza kwa pamoja kwenye soko.

“Hata Kama mnafanya shughuli za mtu mmoja mmoja kwenye mauzo ni muhimu muuze pamoja kwani Ushirika unapandisha hadhi ya mazao na bidhaa na Ushirika ni mwamvuli wa wakulima na ndiyo mtetezi wa wanyonge,” amesema Mhe. Telack. Mkuu wa Mkoa amesema uaminifu na uadilifu ndiyo nguzo ya Ushirika imara hivyo viongozi wakiingia kwenye ushirika waende wakafanye kazi kwa uadilifu na waache mawazo ya kuwa kwenye Ushirika ndiyo kwa kupatia fedha bila utaratibu.

Kwa upande wake Naibu Mrajis - Uhamasishaji, Consolata Kiluma, amevitaka Vyama vya Ushirika Mkoani Lindi kushirikiana na Maafisa Ushirika na Ofisi ya Mrajis Mkoa kujibu hoja za wakulima kwa wakati. Pia Naibu Mrajis amesema, Vyama vya Ushirika Mkoa wa Lindi vimefanikiwa kusajili vyama ila idadi ya wakulima na wanachama wamewasajili wachache hivyo wamalizie kusajili wakulima wao wote wanaowahudumia.

Aidha, Naibu Mrajis ametoa wito kwa wanaushirika wote kuhudhuria kwa wingi Siku ya Ushirika Duniani inayotegemewa kufanyika mkoani Tabora kuanzia tarehe 26/06/2023 hadi 01/07/2023.“Siku ya Ushirika kitaifa ni ya wanaushirika wote na ili ifanikiwe wanachama inabidi mtoe michango na mhudhurie kwa wingi tuendele kuhamasishana tunavyorudi kwani kila Mkoa utakuwa na mabanda yake na tunategemea Ushiriki na michango yenu ili tufanimishe siku hiyo,”amesema Consolata.

## MAAFISA USHIRIKA KANDA YA MASHARIKI WAPEWA MAFUNZO KUIMARISHA USHIRIKA



*Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Collins Nyakunga akimkabidhi cheti cha Mafunzo ya Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika Afisa Ushirika wa Mkoa wa Pwani Vicent Mmary katika Mafunzo yaliyofanyika tarehe 17 – 28 Mei 2023, Mkoani Morogoro*

Maafisa Ushirika wametakiwa kutumia maarifa waliyopata kutokana na programu maalum ya Mafunzo ya Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika iliyoendeshwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa Maafisa Ushirika kutoka mikoa ya Dar es salaam, Pwani na Morogoro.

Maelekezo hayo yametolewa na Naibu Mrajis, Collins Nyakunga, wakati akifunga Mafunzo ya Maafisa Ushirika Mei 28, 2023 Mkoani Morogoro. Mafunzo ambayo yalizinduliwa Mei 17, 2023 na jumla ya Maafisa 72 wamehudhuria na kupata mafunzo ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

Naibu Mrajis amesema lengo la Tume kutoa mafunzo hayo ni kuhakikisha kuwa Maafisa Ushirika wanajengewa uwezo wa kutekeleza majukumu yao vyema ya kusimamia Vyama vya Ushirika ili viweze kujiendesha kwa tija na kupunguza changamoto na ambazo zimekuwepo katika Sekta ya Ushirika.

Sambamba na mafunzo hayo Maafisa Ushirika waliapishwa kutunza Siri mbele ya Hakimu Mkazi Juma Ally Mbonde kwa lengo la kuhakikisha wanasimamia Vyama kwa weledi na kwa kuzingatia maadili ya utunzaji siri ili kuepusha uvujaji wa siri unaoweza kuleta madhara.

Amesema Maafisa Ushirika licha ya Kaguzi wanazofanya mara kwa mara wajikite katika kubaini changamoto na dosari zinazoweza kujitokeza kwenye vyama ikiwemo utatuzi wa migogoro ya vyama pamoja na kufuatilia hoja zinazoibuliwa na Wakaguzi wa nje na kuzifanyia kazi.

Aidha, amewataka Warajis Wasaidizi wa Mikoa pamoja na Maafisa Ushirika kujadiliana masuala ya kiutendaji yanayohusu sekta ya Ushirika kuanzia ngazi za wilaya na mikoa ili pale changamoto zinapobainika ziweze kupata utatuzi wa haraka na pale inapohitajika hatua zaidi taarifa zitolewe na maamuzi yafanyike.

Tume imefanya mafunzo haya ikiwa ni awamu ya tatu, awali mpango huu wa mafunzo ulianza mwaka 2020 katika mikoa ya Kanda ya Kusini na Kanda ya ziwa ambapo maafisa

## WATOA HUDUMA KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA WASIO WAAMINIFU KUFUTIWA LESENI



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege akizungumza wakati wa Ufunguzi wa Mafunzo ya Watoa Huduma wa Vyama vya Ushirika Jijini Dodoma tarehe 01 June, 2023.*

Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt Benson Ndiege, ameagiza kufutiwa leseni Watoa Huduma ambao si waaminifu wanaofanya kazi na Vyama vya Ushirika.

Dkt. Ndiege amesema Watoa Huduma ambao si waaminifu wanatakiwa kufutiwa mara moja leseni zao pale wanapokuwa wanaenda kinyume na kanuni na taratibu za Ushirika na si kusubiri mpaka wamalize muda wao ndiyo wachukuliwe hatua.

Mrajis amesema hayo tarehe 01/06/2023 Jijini Dodoma wakati akifungua mafunzo kwa Watoa Huduma wapya 27 wakusanyaji madeni 12, TEHAMA 6, Bima 2, Huduma za Sheria 3 na Ushauri wa Biashara 4.

Aidha, Dkt Ndiege amesema wapo watoa huduma wenye nia ovu na Ushirika kwasababu wanaingia katika kazi hiyo kwa lengo la kujinufaisha wao na wanasahau kama wao ndiyo daraja la kumaliza chagamoto katika Ushirika na si chanzo cha migogoro.

“Ushirika si chaka la watu wasio na maadili acheni kujiingiza kwenye Ushirika kwa lengo la kutajirika, fanyeni kazi kwa kufuata taratibu na miongozo ya Ushirika kwa maslahi ya wanaushirika hapo Ushirika utafika mbali,” amesema Dkt Ndiege.

Pia Mrajis amesema ni wajibu wa kila Mtoa Huduma kutuma taarifa ya utendaji kazi wake wa kila robo kwa TCDC, lakini wamekuwa hawatoi taarifa hizo na kusababisha kukosekana kwa takwimu za kazi zinazofanywa, hivyo kukosa sifa za kuendelea kufanya kazi na Vyama vya Ushirika.

Wakati huo huo Mtoa Huduma, Dkt Alphonce Massage, kwa niaba ya Watoa Huduma waliohudhuria Mafunzo hayo amesema watakuwa waadilifu na watafanya kazi kwa bidi kwa kufuata miongozo na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

Pia ameishukuru TCDC kwa kuona umuhimu wa kuwaita na kuwapatia mafunzo ambayo yatawajenga katika kazi zao za kila siku na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na Warajis Wasaidizi wa Mikoa.

## SONGWE YAVUNJA REKODI UUZAJI ZAO LA UFUTA KUPITIA STAKABADHI ZA GHALA



*Mkurugenzi Mtendajii wa Halmashauri ya Songwe CPA. Cecilia Kavishe na Viongozi wengine walioshiriki katika Mnada wa nne (4) wa Zao la Ufuta wakijadiliana kuhusu bei ya ufuta katika mnada huo uliofanyika katika Kata ya Magamba wilayani Songwe tarehe 25 Mei, 2023*

Wakulima wa AMCOS 26 katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe Mkoani Songwe wameuza zao la ufuta kwa bei ya juu ya shilling 3,678 kwa kilo katika mnada wa nne (4) wa Ufuta.

uliofanyika tarehe 24/05/2023 katika kijiji cha Magamba Kata ya Totoe Wilayani Songwe Mkoani Songwe.

Akizungumza katika Mnada huo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe,CPA Cecilia Kavishe,amesema kuwa beiya Mnada wa leo imekuwa ni kubwa na imevunja rekodi ikilinganishwa na minada iliyopita ambapo Ufuta uliuzwa kwa shilingi 3,330 kwa kilo moja.

“Bei hii haijawahi kutokea katika minada yote tuliyowahi kuifanya katika Halmashauri yetu na hata katika mikoa mingine hapa nchini, Wakulima wetu wamefurahi na kuzidi kuwa na Imani na “Mfumo wa Stakabadhi za ghala” amesema CPA.Kavishe.

Aidha ametoa wito kwa wakulima ambao bado hawajajiunga na Vyama vya Ushirika kujiunga na Vyama hivyo ili kuweza kupata mikopo na pembejeo kwa urahisi.

Akifungua mnada huo Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ambae pia ni Diwani Kata ya Totoe Mhe.Godian Wangala amewataka wakulima kuendelea kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ilikuweza kuuza mazao kwa bei inayoridhisha na kupata fedha zao kwa wakati.

Mrajis msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa mkoa wa Songwe, Benjamin Mwangwala amewataka wakulima ambao bado hawajajiunga na Vyama vya Ushirika kujiunga na Vyama hivyo ili kuweza kunufaika na faida wanazozipata kupitia Ushirika.

“Sisi kama watendaji tumeelekezwa tuwasaidie wakulima kuuza mazao yao kwa bei ya uhakika ndio maana leo ufuta umeuzwa kwa bei ya juu ya shilingi 3,678 ambayo haikuwahi kutokea kwa mikoa mingine”, amesema Mwangwala.

Aidha, Mwagwala amewataka wanunuzi ambao hawatumii Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kupitia Vyama vya Ushirika kutumia Mfumo huo ili kupata kiwango kikubwa cha mzigo wa mazao na kutokupoteza fedha nyingi kwa madalali.

Naye mmoja wa Wakulima aliyeuza Ufuta kwenye mnada huo, Esther Mwakagali ameishukuru Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Serikali kwa ujumla kuwaletea Mfumo unaowasaidia kuuza mazao yao kiurahisi na kwa bei ya juu inayoridhisha.

“Kabla ya kujiunga na Vyama vya Ushirika na kuanza kuuza Ufuta kwa kupitia Stakabadhi za Ghala tulikuwa tukiuza Ufuta kwa bei anayoitaka mnunuzi lakini kwasasa tunauza kwa bei nzuri sana, mfano soko la leo limetuinua mno tunasema asante sana waliotuletea AMCOS Kata ya Magamba maana tunajua tutapiga hatua tunasonga mbele”.

Mnada huu ni wa nne (4) kufanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe na mnada uliokuwa na bei kubwa ya zao la Ufuta ya shilingi 3678 ikilinganishwa na mnada uliopita ambapo bei ilikuwa ni shilingi 3,330 kwa kilo moja.

CHAMA CHA USHIRIKA NI CHA WANAUSHIRIKA



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Mussa Misaile akikabidhi cheti cha Usajili cha Chama kipya cha Ushirika wa Mbogamboga, matunda na mazao mchanganyiko Mang'ola AMCOS kwa Mwenyekiti wa Chama Athuman Salum baada ya mafunzo ya Ushirika, Jijini Arusha tarehe 5 June, 2023*

Wanachama wa Chama cha Ushirika wametajwa kuwa ndio wamiliki wa kwanza wa Chama cha Ushirika. Hivyo, wana wajibu wa kulinda na kusimamia Chama cha Ushirika kuendeshwa kwa tija kwa maslahi ya Wanachama wote wa Chama cha Ushirika.

Hayo yamebainishwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Mussa Musaile akifunga mafunzo yaliyoratibiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Bodi wa Vyama vipya vya Ushirika kutoka Halmashauri za Wilaya za Karatu, Meru na Arusha wanaolima mazao ya Mbogamboga, matunda na mazao mchanganyiko yaliyoanza Juni 5, 2023 na kuhitimishwa Juni 6, 2023 Mkoani Arusha.

Katibu Tawala amewaasa Viongozi kwenda kusimamia na kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha kwamba wanasimamia wanachama wao kutimiza wajibu wao ikiwemo ulipaji wa hisa utakao changia katika kujenga na kuimarisha mtaji wa Chama, kulipa viingilio, kushiriki wa Mikutano mikuu, Chaguzi za Vyama pamoja na majukumu mengine yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Masharti ya Chama.

“Vyama vya Ushirika vinamilikiwa na wanachama wenyewe, hivyo ili kuhakikisha vyama hivi vinakuwa imara na endelevu ni lazima kila mwanachama ahakikishe anamaliza hisa kwa mujibu wa Sheria na Masharti ya Chama ili kuweza kujenga mtaji wa ndani wa chama na kuwa imara kiuchumi,” alisema

Aidha, Katibu Tawala amewasihi Viongozi hao kutumia maarifa waliyopata kutekeleza kwa vitendo na kuhakikisha wanachama wanaendeleza kilimo cha mbogamboga, matunda na mazao mchanganyiko kwa maendeleo yao wenyewe na kwa jamii inayowazunguka. Akaongeza kuwa kupitia Vyama vya Ushirika Wajumbe wa Bodi watumie fursa za zilizopo katika Kilimoikiwemo masoko, makongamano, ziara za kibiasharana pembejeo za kilimo kwa ustawi wa Vyama vya Ushirika.

Awali akiongea kwa niaba ya washiriki wa mafunzo John Mangi ameishukuru Serikali kwa kuendelea kutenga fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya masuala ya Kilimo pamoja na kuusimamia Ushirika Mshiriki huyo amesema Wanaushirika wana matarajio makubwa ya upatikanaji wa masoko kupitia Ushirika hususani kwa mazao yanayozalishwa na wakulima wa mazao ya Mbogamboga, matunda na mazao mchanganyiko. Hivyo, wajumbe hao wataenda kuzingatia masuala mbalimbali yaliyofundishwa kwa lengo la kuwa na Ushirika imara.

Aidha, ameiomba Serikali kuendelea kutoa mafunzo kwa wanaushirika ili kuimarisha na kusimamia Ushirika pamoja na uwezekano wa kuongeza mbolea ya Ruzuku kwa

Wakulima hususani kwa maeneo yaliyo mbali na miji sambamba na mbolea hiyo kuzingatia aina ya zao na eneo la kilimo.

Aidha, mshiriki huyo ameiomba Serikali kujenga miundombinu ya maghala ya kisasa, mashine za kuchakata na kusindika mazao, miundombinu ya kuvuna na kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji na Barabara kwenye maeneo ya mashamba.

Jumla ya Vyama vya Ushirika wa mazao ya Mbogamboga, matunda na mazao mchanganyiko 14 vimeanzishwa mkoani Arusha ambapo Wajumbe wa Bodi wapatao 86 wamepata mafunzo. Timu za wataalamu kutoka taasisi mbalimbali ikiwemo Wizara ya Kilimo, Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), TAHA, wametoa mada mbalimbali ikiwemo dhana ya Ushirika, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Wajibu wa Wajumbe wa Bodi, Maadili ya Uongozi, Uendeshaji wa Mikutano Mikuu ya Vyama, Uandaaji wa makisio ya mapato na matumizi ya Chama pamoja na upatikanaji wa pembejeo.

## WAZIRI SIMBACHAWENE AZINDUA MIKATABA YA HUDUMA KWA MTEJA YA TAASISI ZA UMMA, UKIWEMO WA TCDC



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akiongea wakati wa Uzinduzi wa Mikataba ya Huduma kwa Mteja kwa Taasisi za Umma uliofanyika Jijini Dodoma tarehe 23 Juni, 2023*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene Juni 23, 2023 amezindua Mikataba ya Huduma kwa Mteja ya Taasisi za Umma, ukiwemo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akimkabidhi Mkataba wa Huduma kwa Mteja Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa TCDC Gabriel Mwita wakati wa Uzinduzi wa Mikataba ya Huduma kwa Mteja kwa Taasisi za Umma uliofanyika Jijini Dodoma tarehe 23 Juni, 2023*

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika Jijini Dodoma, Mhe.Simbachawene amezitaka Taasisi zote za Umma kuwa na Mikakati ya Huduma kwa Mteja iliyo hai na kujenga uelewa kwa wateja kuhusu Mikataba ya Huduma kwa Mteja; na Utekelezaji wa Majukumu yake.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizinduaMikataba ya Huduma kwa Mteja kwa Taasisi za Umma uliofanyika Jijini Dodoma tarehe 23 Juni, 2023*

Mkataba wa Huduma kwa Mteja unalenga kuwawezesha Watumishi wa Umma kuongeza uwajibikaji na nidhamu ya kazi; kuwa na utamaduni wa utendaji kazi unaojali matokeo natija kwa wakati; kutenda kazi kwa usikivu na uadilifu; na kuimarisha mahusiano ya kikazi baina ya Watumishi wa Umma na wateja na wananchi kwa ujumla.

## SERIKALI KUIMARISHA SEKTA YA USHIRIKA



*Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. David Silinde akikata Utepe wa Uzinduzi wa Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani katika viwanja vya Nanenane – Ipuli Mkoani Tabora tarehe 27 Juni, 2023*

Serikali imesema imedhamiria kuimarisha na kuendeleza azma yake ya kuimarisha, kusimamia na kuendeleza Sekta ya Ushirika nchini kwa lengo la kuondoa umaskini na kujenga uchumi imara wa Wananchi.

Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mhe. David Silinde kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Hamis Ulega ameyasema hayo wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Juni 27, 2023 katika Viwanja vya Nanenane Ipuli Mkoani Tabora.

Naibu Waziri amesema Serikali ina azma ya kuimarisha Ushirika kutokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea ikiwemo kuimarisha na kukamilisha kanzidata na kusajili Wakulima nchini ili taarifa hizo ziweze kusaidia katika usimamizi wa Ushirika, usambazaji wa pembejeo na Viwatilifu kwa lengo la kuongeza uzalishaji na hatimaye kukuza masoko kupitia Ushirika.

“Sote tunatambua mchango wa sekta ndogo ya ushirika katika nchi yetu hasa katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi wa nchi. Nipende kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania inatambua kwamba, ushirika unasaidia watanzania hasa wenye kipato cha chini katika kukabiliana na umasikini" alisema

Aidha, amekitaka Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU) kuendelea kutoa mafunzo ya Ushirika kwa Wanaushirika, Wadau na Umma ili Wananchi wengi waweze kuelewa Ushirika, kutambua fursa za kiuchumi zilizopo katika Sekta ya Ushirika na kuzitumia kuondoa umaskini.

Aidha, amesema kutokana na takwimu zilizotolewa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) kuonesha idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka wanachama 6,965,272 Desemba, 2021 hadi 8,358,326 kufikia Machi, 2023. Ongezeko hilo limetokana na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa kujiunga na ushirika. Hivyo, suala kubwa ambalo Serikali inalisisitiza ni kuhakikisha wakulima, wafugaji na wavuvi wengi wanajiunga kwenye vyama vya ushirika.

Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Irene Madeje kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamisheni Abdulmajid Nsekela amesema miongoni mwa vipaumbele vya kuimarisha Ushirika vya Tume ni pamoja na kuimarisha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika usimamizi na uendeshaji wa Vyama hasa kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika unaosimamiwa na Tume.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege amesema Tume imeendelea kusimamia Sekta hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha kaguzi katika Vyama, kuvunja Bodi za Ushirika pale inapohitajika, kutoa mafunzo na kuhamasisha uanzishaji wa Vyama, pamoja na kuhamasisha Amcos kuanzisha SACCOS.

Ufunguzi huo umehudhuriwa na Viongozi mbalimbali wakiwemo Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Tabora, Mwakilishi wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika Zanzibar Zainab Hassan, Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Wanaushirika pamoja na Wadau wa Ushirika. Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika 2023 ni "Ushirika kwa Maendeleo endelevu.

## STAKABADHI ZA GHALA KUPAISHA USHINDANI WA SOKO KWA MAZAO YA WAKULIMA



*Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe akisaini Kitabu cha wageni waliotembelea banda la Ushirika Siku ya Stakabadhi za Ghala kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika katika Viwanya vya Nanenane – Ipuli Mjini Tabora tarehe 28 Juni, 2023.*



*Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe akiwa katika banda la Ushirika Siku ya Stakabaddhi za Ghala kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika katika Viwanya vya Nanenane – Ipuli Mjini Tabora tarehe 28 Juni, 2023.*

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe, ametoa wito kwa kila Mdau anayehusika katika matumizi na usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kutimiza wajibu wake katika nafasi yake ili kupata masoko ya mazao ya wakulima yenye ushindani.

Mhe. Kigahe ameyasema hayo Juni 28, 2023 wakati wa Siku ya Stakabadhi ya Ghala kwenye wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani iliyoanza Juni 26, 2023 na kilele cha Maadhimisho hayo kitakuwa Julai 01, 2023 katika Viwanja vya Nanenane Mjini Tabora.

Amesema matumizi ya Stakabadhi za Ghala yana umuhimu katika kukuza sekta ya biashara na masoko ya bidhaa nchini. Hivyo, wadau wanaohusika na Mfumo huu wakiwemo wakulima, watendaji katika Vyama vya Ushirika, wasimamizi wa maghala kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Stakabadhi za Ghala ili kukuza ushindani wa soko kwa kuwapa wakulima bei nzuri yenye tija.

“Kama mnavyofahamu, Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unajumuisha wadau mbalimbali wakiwemo Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Waendesha Ghala, Mameneja Dhamana, Wakulima na Wazalishaji wa bidhaa nyingine, Taasisi za Fedha, Kampuni za Bima, Wakaguzi wa Ghala, Vyama vya Ushirika na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Ufanisi katika kufikia malengo ya Mfumo wa unategemea utekelezaji wa wajibu wa kila mdau,” alisema Mhe Kigahe.

.

## USHIRIKA WETU UWE IMARA, WENYE KUKUZA UCHUMI - DKT.CHUACHUA




*Mkuu wa wilaya ya kaliua mkoani Tabora, Dkt. Rashid Chuachua, akimkabidhi tuzo ya SACCOS bora kwa Afisa Huduma kwa wateja (TANESCO) Rose Mugoo wakati wa maadhimisho ya siku ya ushirika duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Na ya nenane- Ipuli mjini Tabora tarehe 30 Juni, 2023*

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, Dkt. Rashid Chuachua,amewaasa wanaushirika kutumia Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani kujitafakari na kuangalia Sheria, Sera, Kanuni na Taratibu ili kutumia Ushirika kwenye kukuza uchumi wa nchi.

Dkt.Chuachua ametoa kauli hiyo Juni 30, 2023 mjini Tabora kwenye Kongamano la Wanaushirika lililokuwa na lengo la kujadili maeneo yanayohitaji kufanyiwa maboresho na kuishauri Serikali.

Amesema ni muhimu maadhimisho hayo yakatumika kuangalia maeneo hayo ili kujiimarisha na kujiletea maendeleo endelevu ya ushirika nchini.

“Nikupongeze Mrajis kwa kazi unayofanya ya kusimamia Ushirika nchini, dhamira ya Serikali ni kuona Ushirika unakuwa na maendeleo endelevu katika shughuli za uchumi na jamii yanafikiwa, hii ni sekta mtambuka yenye kusimamia uchumi wa nchi na kuongeza pato la taifa na kukuza uchumi wa mwanachama mmoja mmoja,” amesema.

Aidha, amesema maadhimisho hayo yanatoa dira na mwelekeo wa kuisaidia Wizara kutatua changamoto zilizopo leo ili kesho zisiwepo tena na kwamba maadhimisho hayo lazima yatoe matokeo yanayopimika ili kuona manufaa yake.

Kadhalika, amesema kuna tatizo la weledi wa taaluma ya hesabu kwa watumishi wa vyama vya ushirika na kupongeza Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuwa na mafunzo mbalimbali yanayotolewa bila kuzingatia viwango vya elimu ili kuwa na ufanisi kwenye hesabu za ushirika.

Awali, amesema wanaushirika wamejengewa uwezo kupitia makongamano mbalimbali ikiwamo masuala ya kodi, elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa, masoko ya bidhaa na huduma na ukaguzi katika vyama vya ushirika kufikia maendeleo endelevu.

“Mmeshiriki kongamano la biashara na uwekezaji kwa vyama vya ushirika kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Nafasi ya Ushirika kuanzisha viwanda vidogo vidogo pamoja na fursa ya uwekezaji katika hisa za benki, vipande na soko la mitaji kukuza fursa za uwekezaji, pia kongamano la Sekta ya Huduma za Fedha na TEHAMA ikiwa na uzoefu katika huduma za kifedha za benki na SACCOS pamoja na Ushirika kujiendesha kidigitali ikiwa ni pamoja na matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa vyama vya ushirika ili kuleta maendeleo endelevu,” amesema.

Naye, Mrajis wa Vyama Vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege amesema Tume hiyo inaendelea kutekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika eneo la Ushirika kutokana na kuwekewa msisitizo kwa kutajwa mara 85.

“Kongamano hili limetokana na majukwaa ya Ushirika kwenye mikoa, kuna suala la vyama vingi vya Ushirika wa mazao kwa mfano Tumbaku tuna vyama vya kilimo lakini baada ya mauzo wananchi hawapati namna ya kutunza fedha zao na mwisho wa siku fedha zinaisha na inapofika mwisho wa msimu wanarudi kwenye utumwa wa kukopa; hapa wameongea kuhusu Benki ya Ushirika na kuweka mikakati, kuhusu Stakabadhi za Ghala, sera na sheria ya Ushirika na Ushirika kufanya kazi kibiashara,” amesema.

# VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO VYAASWA KUTOAELIMU



*Mkurugenzi wa Sekta ya Fedha Kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Saadat Musa akikagua mabanda ya ushirika katika siku ya Ushirika Duniani yaliofanyika katika viwanja vya Nanenane- Mkoani Tabora tarehe 29 Juni, 2023*

Mkurugenzi wa Sekta ya Fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Saadat Musa ametoa wito kwa Vyama vya Ushirika kutoa elimu ya Fedha kwa Wanachama na Umma kwa ujumla kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Fedha mjini na Vijijini.

Ameyasema hayo akimwakilisha Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, Juni 29, 2023 wakati akiongea na Wanaushirika katika siiku ya Huduma za Fedha na TEHAMA katika Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yanayoendelea katika Viwanja vya Nanenane Ipuli Mjini Tabora.

Amesema Vyama vya Ushirika vina wajibu wa kuelimisha Wanachama wake ili wawe na uelewa sahihi wa elimu ya fedha, uwekezaji na huduma jumuishi za kifedha (financial inclusion). Hivyo, kuwawezesha kuimarisha mapato yao na mitaji ya Vyama vyao.

Aidha, ametoa Rai kwa Wanaushirika kutekeleza na kukamilisha taratibu za kuanzisha Benki ya Ushirika na kuongeza kuwa Serikali kupitia Benki kuu iko tayari kutoa ushirikiano wa kuanzisha Benki hiyo kwa kutoa miongozo na taratibu za kuanzisha Benki hiyo.

Kwa upande wake Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt Benson Ndiege, amevitaka Vyama vya Ushirika ambavyo bado havijaomba Leseni ya Uendeshaji kufanya hivyo ili kuendana na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 na kuepukana na adhabu.

## MICHEZO YA MAADHIMISHO YA SIKU YA USHIRIKA YAFANA



*Timu ya Netiball ya TCDC ikiwa kwenye bonanza la michezo kuelekea siku ya Ushirika Duniani lililofanyika katika viwanja vya Chuo cha Utumishi wa Umma Mjini Tabora tarehe 29 Juni, 2023*

Bonanza lafanyika kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani Julai mosi mwaka 2023 ambapo michezo mbalimbali imechezwa katika Viwanja vya Chuo cha Utumishi wa Umma Mjini Tabora.

Michezo ambayo imepigwa Juni 29, 2023 ni soka, netiboli kuvuta kamba na kukimbiza Kuku ikiwakutanisha wafanyakazi na watumishi wa Ushirika na Shirikisho la vyama vya Ushirika.

Mwenyekiti wa Kamati ya ndogo ya Michezo, Burudani na Matangazo ya maandalizi ya maadhimisho ya siku ya ushirika Duniani, Ibrahim Kadudu amesema michezo hiyo ilifanyika katika uwanja wa Chuo cha Uhazili.

Amesema timu zilizoshiriki michezo hiyo ikijumuisha wachezaji kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU).

"Ushirika asili yake ni mashirikiano na michezo yote asili yake ni mashirikiano hakuna mchezo ambao unaweza kuchezwa na mtu mmoja inachezwa na zaidi ya moja," amesema Mwenyekiti huyo.

Amesema faida zinazopatikana ni pamoja na mahusiano na uchumi kwa watu mbalimbali. "Niwasisitize wanaushirika michezo ni eneo la muhimu kuimarisha afya na watumishi tuendelee kufanya mazoezi hata baada ya bonanza hili,"amesema Kadudu

Pamoja na mambo mengine washindi walioibuka kukimbia kwenye gunia ni Issa Ahamed na Agustino Abdul Karim kutoka TCDC, kukimbia kuku Issa ameendelea kubaki mshindi akifuatiwa na Raphael. Nae Adolf Ndunguru akifuatiwa na Noel Steven washindi kipindi cha pili wakitokea TCDC.

Aidha, mchezo wa mpira wa Pete Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) ilishinda kwa magoli 30 dhidi ya TCDC iliyopata magoli 10. Mgeni Rasmi Mrajis Msaidizi wa Geita Doreen Mwanri ametoa zawadi ya mipira Kwa timu za Netiboli kuunga mkono juhudi za wanamichezo.

## USHIRIKA WA PAMOJA WA WACHMBAJI MADINI YA DHAHABU WAANZISHWA



*Mrajis msaidizi Mkoa wa Shinyanga Hilda Boniphace akiongea wakati akizindua Mkutano Mkuu wa kwanza wa Uchaguzi wa Ushirika wa pamoja wa wachimbaji madini yaDhahabu (KAMIKOJE) uliofanyika wilayani Kahama Mkoani Shinyanga tarehe 13 June, 2023*

Wachimbaji wa Madini ya Dhahabu Wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga wametakiwa kuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na Serikali katika kutatua changamoto ambazo zitakuwa zikiwakuta katika utendaji wao wa kazi za uchimbaji.

Ushirika haukatazwi hata mkiamua kumiliki mgodi kwani inatakiwa kufuata utaratibu ambazo utatakiwa kufanya ikiwa na lengo kunakuwa na mabadiliko makubwa katika kujiingizia kipato.

Hayo yalibainishwa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Shinyanga,Hilda Boniface,tarehe 13 Juni,2023 wakati akizindua Mkutano Mkuu wa Kwanza wa uchaguzi wa Ushirika wa pamoja wa Wachmbaji madini ya dahahabu (KAMIKOJE) ulifanyika Wilayani Kahama.

Boniface alisema kuwa umoja huo ambao unajumuisha vyama vya IGOMICO, KAMICOSO, BMS, KAMICOS na MKAMICO anawapongeza kwa kufikia hatua ya kuunda ushirika kwani hatua kubwa ambayo wamefika na kuongeza sio rahisi kwa wengi kufika.

Alisema kuwa umoja huo unalenga katika kutatua changamoto ambazo zitakuwa zikiwakabili wachimbaji hao huku akiongeza kuwa cheti ambacho atawapa ni kuutambulisha mradi huo wa pamoja wa wachimbaji wa dhahabu waliopo.

Aidha, Boniface aliwataka Maafisa Ushirika kuendelea kutoa elimu ya Ushirika kwa wachimbaji wa madini ya dhahabu kila siku ili kuhakikisha kuwa wanaufahamu Ushirika kwa hali ya juu ili kuona wanakuwa na mabadiliko katika sekta hiyo ya madini.

Alisema kuwa uchaguzi wa viongozi wa Ushirika huo utazingatia misingi ya kisheria kwani taasisi hiyo iliyoanzishwa ni kubwa inaweza kuitwa popote pale hivyo viongozi watakaochaguliwa lazima wawe watu anaojielewa na kipaji cha uongozi.

Aliwataka wote watakaochaguliwa watapewa semina elekezi za uongozi ili kupata uwezo wa kuweza kuwaongoza wanachama na kuongeza atahamasisha wachimbaji wengine katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji Mkoa wa Shinyanga kuhakikisha kuwa wanaunda ushirika kama huu uliopo.

Katika uchaguzi huo ambao ulijumuisha wagombea 10 wakiwemo wajumbe wa Bodi, Asha Msangi alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Ushirika huo huku Makamu Mwenyekiti akiwa Cosmas Paul ambao kwa mujibu wa sheria watatakiwaa kuongoza kwa kipindi cha Miaka mitatu.

# MAAFISA USHIRIKA KAGERA WATAKIWA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA'MUVU'




*Maafisa Ushirika na Watendaji wa vyama wa mkoa wa Kagera wakiwa kwenye Mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa vyama vya Ushirika (MUVU) yaliofanyika Mkoani Kagera tarehe 19 Juni, 2023*

Maafisa Ushirika wametakiwa kusimamia matumizi ya Mfumo wa TEHAMA wa Usimamizi wa vyama vya Ushirika 'MUVU' kwa lengo la kuhakikisha mnyororo wa uzalishaji na ukusanyaji wa mazao unafanyika kwa usahihi na Mkulima anapata malipo sahihi na kwa wakati.

Ameyasema hayo Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika anayesimamia Masoko na Uwekezaji, Revocatus Nyagiro, wakati wa kikao cha mafunzo ya Usimamizi wa Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa Maafisa Ushirika na Watendaji wa Vyama yaliyoratibiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa lengo la kukuza uelewa wa matumizi ya Mfumo huo kilichofanyika Bukoba Mkoani Kagera Juni 19, 2023.

Amefafanua kuwa ni wajibu wa Maafisa Ushirika kuhakikisha kuwa wanawapa watendaji wa Vyama vya Ushirika ushirikiano wa kutosha wa kutumia na kuelewa Mfumo huo wa Usimamizi katika hatua za ukusanyaji wa mazao kutoka kwa wakulima, uandaaji wa taarifa sahihi za mazao kwenye ghala, uuzaji na mkulima kupata mrejesho katika kila hatua kwa njia ya ujumbe mfupi wa Simu.

## RC DODOMA ATAKA USHIRIKA ULETE MAPINDUZI KIUCHUMI




*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyemule akiongea katika jukwaa la Maendeleo ya Ushirika jijini Dodoma tarehe 19 Mei, 2023*

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amevitaka vyama vya Ushirika kutumia fursa za kiuchumi kunufaisha Wanachama na kuongeza tija ili kuongeza vipato vya wanachama na maendeleo ya Vyama na pato la Taifa kuongezeka.

Akizindua Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dodoma, Mei 19, 2023 katika Viwanja vya 'Nyerere Squire' amesema Vyama vya Ushirika vitumie fursa zilizopo katika kilimo, mifugo, uvuvi, mabwawa ya umwagiliaji, mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha pamoja na ushirikiano uliopo kutoka Serikalini.
Amesema Serikali inahimiza Ushirika kwakuwa ni moja ya nyenzo ya kusaidia wananchi kuunganisha nguvu kwa pamoja, kupata huduma za pamoja na kutatua changamoto zao kiuchumi na kuondoa umasikini.

Hivyo, Vyama vya Ushirika kama sekta binafsi vijiendeshe kibiashara na kufanya uwekezaji utakaoleta faida kwa Vyama na kukuza uchumi.
Aidha, amesema Mkoa wa Dodoma una fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo utalii, kilimo cha mazao ya kimkakati ya zabibu, alizeti, Korosho, Mtama pamoja na mazao mengine ambazo zikitumika kimkakati vitasaidia vyama vya Ushirika kuimarika na kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

Sambamba na azma hiyo, Mkuu wa Mkoa ameagiza Waajiri kuwasilisha makato ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ya watumishi wao kwenye vyama husika vya Ushirika kwa wakati kwa mujibu wa Sheria Na.10 ya Huduma Ndogo za Fedha (2018).

Kwa upande wake Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege, amewakumbusha Wanaushirika kuzingatia majukumu ya Wanachama katika vyama vya Ushirika ili vyama viweze kuendelea kuwa imara na kuleta tija kwa kushiriki kikamilifu katika Chaguzi za Vyama, Mikutano Mikuu pamoja na majukumu mengine yaliyowekwa kisheria.

Aidha, Mrajis ametoa rai kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama kuzingatia utunzaji bora wa taarifa za Vyama hususani kuvisajili vyama katika Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), akisisitiza Vyama kujisajili katika Mfumo huo ifikapo Mei 31, 2023 ili kurahisisha utaratibu wa utunzaji na taarifa sahihi za Vyama vya Ushirika.

Jukwaa hilo limeambatana na Maonesho ya bidhaa na huduma za Vyama vya Ushirika, utoaji wa Vyeti kwa vyama vya Ushirika vilivyoshiriki kikamilifu katika Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dodoma 2023 pamoja na maandamano ya Jukwaa yaliyofanyika Jijini Dodoma.

## WANAUSHIRIKA WATAKIWA KUFANYA KIKAO NA WIZARA YA FEDHA NA TRA ILI KUJADILI CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI




*Mwenyeketi wa Kamisheni ya Tume la maendeleo ya Ushirika, Akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi na Wadau wa Ushirika katika jukwaa la maendeleo ya Ushirika jijini DAR-ES-SALAAM tarehe 11 Mei, 2023*

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya ushirika, Abdulmajid Nsekela amewataka Shirikisho la Vyama vya Ushirika Nchini (TFC), Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SCCULT), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kuandaa Kikao kati yake na Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kujadili na kutafuta suluhu ya changamoto zinazowakabili Wanaushirika.

Amesema kikao hicho kitasaidia kuboresha mahusiano mema kati ya taasisi hizi na Wanaushirika ili kuwapa ahueni Wanashirika katika uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, ikiwemo Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo SACCOS.

Bw. Nsekela amesema hayo katika Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dar es salaam lililofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 11/5/2023 likiwa na Kauli Mbiu inayosema “Ushirika kwa Maendeleo Endelevu”

Vilevile, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Ushirika amesema kumekuwa na shida ya mitaji katika vyama katika kujiendesha kibiashara na kuwa na Ushirika endelevu, ameviomba Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo kuona namna vinavyoweza kushirikiana na

Ushirika wa aina nyingine kwa kuwasaidia mitaji itakayowawezesha kupata pembejeo na mitaji kwaajili ya uendeshaji wa shughuli za Ushirika.
Aidha, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Ushirika amevitaka Vyama kufuata taratibu na Sheria ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika uhamasishaji wa uanzishwaji wa Vyama.

"Wapo viongozi wachache ambao wanaendesha Vyama vyao bila kufuata taratibu sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, hawa hatutawavumilia," amesema Nsekela.

Akizungumza katika Jukwaa hilo Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege amesema SACCOS zote ambazo hazijaomba leseni zinapaswa kusitisha biashara zao mpaka pale zitakapoomba leseni husika kwa mujibu wa matakwa ya Sheria.

Dkt. Ndiege amesema mambo yote ya Leseni (ikiwemo leseni za muda), maombi ya kufungua matawi, milango ya huduma, uwasilishaji wa Taarifa za utendaji wa SACCOS za kila mwezi na robo mwaka pamoja na aina nyingine ya shughuli za SACCOS, yanapaswa kuwasilishwa kwa njia ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ili yaweze kushughulikiwa kwa haraka.

"Inawezekana mnaendesha SACCOS zenu bila leseni, hili ni kosa la Jinai kuendesha biashara ya Huduma Ndogo za Fedha pasipo kuwa na Leseni ya kufanya biashara ya Huduma Ndogo za Fedha nchini," amesema Dkt. Ndiege.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam, Mussa Chowo ameomba Serikali kupunguza Kodi ya Mapato inayolipwa na Vyama vya Ushirika kutoka asilimia 30 hadi asilimia 10.

## WANAUSHIRIKA WATAKIWA KUWA WAADILIFU KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA



*Mkuu wa mkoa wa Geita, Mhe.Martin Shigela akizungumza katika jukwaa la maendeleo ya Ushirika Mkoani Geita tarehe 5 Mei, 2023*

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhe. Martine Shigela amewataka Viongozi na Wanaushirika kuwa Waadilifu katika vyama vyao.

Mhe. Shigela ameyasema hayo alipokuwa akifungua Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Geita tarehe 5/5/2023 Wilaya ya Geita.

Amesisitiza Uadilifu kwa Wanaushirika ili kusaidia Vyama na Wakulima kuepuka Hasara na kufa kwa Vyama kama yaliyotokea miaka ya nyuma, pia kuboresha huduma mbalimbali kwenye vyama hivyo ili kuvutia ambao hawapo katika Vyama vya Ushirika kuweza kujiunga kwa wingi.
“Serikali ya Mama Samia haitakubali kurudi huko tena la muhimu ni kufuata misingi ya Ushirika inavyosema,“ alisema Shigela.

Umuhimu wa vyama vya Ushirika ni kuirahisishia Serikali kuweza kuwahudumia Wakulima wengi kwa urahisi hata katika ugawaji wa pembejeo.

Aidha katika suala la Usajili wa Vyama katika mfumo lizingatiwe na kama kuna changamoto zisemwe sasa kama kuboreshwa waboreshe sasa ili utapoanza kufanya kazi ambaye hatajisajili atahesabika kama Mkaidi.

## MICHEZO YA MEI MOSI 2023 YAZINDULIWA




*Watumishi wa TCDC, wakiwa katika maandamano ya uzinduzi wa Michezo ya Kombe la MeiMosi, mjini Morogoro tarehe 01 Mei,2023*

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Fatma Mwasa amezindua rasmi michezo ya Kombe la Mei Mosi 2023 katika Viwanja vya Jamhuri Mkoani Morogoro iliyoshirikisha Watumishi wa Umma kutoka taasisi mbalimbali za Serikali.

Akifungua Maadhimisho hayo Mkuu wa Mkoa amesema Michezo ni muhimu kwa Taasisi na Watumishi kuzingatia masuala ya michezo ili kuhakikisha kazi zinafanyika kwa ufanisi na kasi ya utekelezaji wa majukumu inaongezeka.

Aidha, katika ufunguzi huo Timu ya Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika 'TCDC Ushirika Sport' imecheza mpira wa miguu dhidi ya Timu ya Watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani na kufanikiwa kutikisa Nyavu kwa matokeo ya Bao 1 kwa 2 katika muendelezo wa Mechi za mtoano za Mashindano hayo yaliyofanyika Viwanja vya Mazimbu.

Katika hatua nyingine za mashindano hayo 'TCDC Ushirika Sport' imecheza Mpira wa wavu wa Wanaume na Timu ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kupata Seti 0 kwa Seti 2. Mashindano hayo mwaka huu yanapambwa kwa kauli Mbiu***"Miaka Miwili ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Imeimarisha Michezo na kuongeza Ufanisi Kazini, Kazi Iendelee".***

## KUTUMIA TEHAMA KWENYE SEKTA YA KILIMO KUNAPUNGUZA GHARAMA ZA UENDESHAJI - ENG. NDOMBA



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandaoni (e-GA), Eng.Benedict Ndomba akizungumza katika uzinduzi wa kikao cha kujadili jinsi ya kuunganisha Mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Kilimo kilichofanyika jijini Dodoma tarehe 23 Machi, 2023*

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Eng. Benedict Ndomba amesema kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye Sekta ya kilimo kunapunguza gharama za uendeshaji na kuhakikisha mipango ya muda mfupi na muda mrefu inaenda kama ilivyopangwa.



*Washiriki wa kikao cha Maafisa na Wataalam wa TEHAMA wakimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandaoni (e-GA), Eng.Benedict Ndomba katika kikao kazi cha kujadili jinsi ya kuunganisha Mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Kilimo kilichofanyika Jijini Dodoma tarehe 23 Machi, 2023*

Hayo yamebainishwa na Eng. Ndomba wakati akifungua kikao Kazi cha kujadili jinsi ya kuunganisha Mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Kilimo nchini kupitia Wizara ya Kilimo cha kilichoandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kilichofanyika tarehe 23/03/2023 Jijini Dodoma.

Naye mwakilishi kutoka Wizara ya Kilimo, Sixtus Tope ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, ameishukuru TCDC kwa kuandaa kikao Kazi kilichowakutanisha wataalamu wa mifumo ya TEHAMA iliyopo chini ya Wizara ya KiIimo.




*Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika Wilayani Kondoa Mkoani Dodoma tarehe 8, Machi, 2023*

# WANAWAKE TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA WASHIRIKIMAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI



*Watumishi Wanawake wa TCDC wakiwa katika maandamano ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kimkoa Wilayani Kondoa Jijini Dodoma tarehe 8 machi, 2023*

Wanawake kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) wameshiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kwa mkoa wa Dodoma yamefanyika katika wilaya ya Kondoa.

Maadhimisho hayo yaliyofanyika tarehe 08/03/2023 Mgeni Rasmi alikuwa ni Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule.

Kauli Mbiu ya Maadhimisho hayo ni "**Ubunifu wa Mabadiliko ya Kiteknolojia; Chachu katika kuleta Usawa wa kijinsia"**

# VYAMA VIKUU MTWARA VYAKABIDHI MILIONI 253 KUSAIDIA HUDUMA ZA KIJAMII




*Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe.Kanali Ahmed Abbas akipokea Hundi ya milioni shilingi 153 kutoka Chama Kikuu cha MAMCU LTD kwa ajili ya kuchangia huduma za jamii tarehe 2 Februari, 2023*




*Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas akipokea Hundi shilingi milioni 50 kutoka kwa Chama Kikuu cha TANECU LTD kwaajili yakuchangia za huduma za jamii mjini Mtwara tarehe 2 Februari, 2023*

Vyama Vikuu vya Ushirika mkoani Mtwara vimekabidhi Shilingi millioni 253 Kwa Mkuu wa Mkoa huo, Kanali Ahmed Abbas kwa ajili ya kuchangia huduma za jamii.

Fedha hizo zimekabidhiwa Mjini Mtwara tarehe 02 Februari,2023 na Chama Kikuu cha Ushirika cha Masasi na Mtwara (MAMCU LTD) Shilingi Milioni 203 kwaajili ya Elimu, Afya na Maji;na Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala (TANECU LTD) Shilingi milioni 50 kwaajili ya Elimu.

Vyama hivyo vimekabidhi fedha hizo ikiwa ni kurudisha shukrani kwa wananchi na Serikali baada ya msimu wa mazao wa mwaka 2022/2023 kumalizika kwa Mafanikio.

## MAMCU YAUNGA MKONO 'BLOCK FARMING'




*Trekta mbili zinazomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Masasi na Mtwara (MAMCU LTD) kwaajili ya Kilimo cha mashamba makubwa (Block Farming)*

Chama Kikuu cha Ushirika cha Masasi na Mtwara (MAMCU) kimeanza kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuanzisha Kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja (block farming) ambapo hadi sasa kinamiliki mashamba hekari 750 na Trekta mbili kwaajili ya Kilimo hicho.

Mwenyekiti wa MAMCU, Siraji Mtenguka, amesema Februari 02, 2023 kuwa mashamba hayo yanaandaliwa kutumika kwaajili ya kulima mazao ya Korosho pamoja na Ufuta na yatamilikiwa na Wanaushirika.

# VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA MKOANI LINDI VYAPONGEZWA KWA KUWALIPA WAKULIMA KWA WAKATI




*Ofisi za Chama Kikuu cha Ushirika cha Ruangwa, Nachingwea na Liwale (RUNALI COOPERATIVE UNION)*

Kaimu Naibu Mrajis (Uhamasishaji na Uratibu), Consolata Kiluma, amevipongeza Vyama Vikuu vya Ushirika Mkoani Lindi, vya Lindi Mwambao na RUNALI kwa kuwalipa wakulima fedha zao za mauzo kwa wakati katika msimu wa mwaka 2022/2023.

"Niwapongeze kwa kuwalipa wakulima, Wanaushirika na wasiokuwa wanaushirka kwa kuwalipa fedha zao kwa wakati baada ya msimu wa mauzo kuisha, hii inajenga imani kwa wakulima kuendelea kupata moyo wakuweza kulima zaidi na kupata faida kubwa zaidi," amesema Kiluma.

Aidha, amewataka wakulima ambao hawako kwenye Vyama vya Ushirika kujiunga na Vyama hivyo ili kunufaika na fursa zilizopo kwenye Ushirika ikiwa ni pamoja kuuza mazao kwa mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

Vilevile, Naibu Mrajis amevitaka Vyama hivyo kuendelea kufanya uwekezaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji, kujenga maghala, kununua magari na kujenga ofisi, kuwa na hati miliki za mali wanazozimiliki ili mali za vyama zisipotee.

## USHIRIKA NA MFUMO WA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA

Katika Jamii kuna shughuli mbalimbali ambazo binadamu huwa anazifanya kila siku kwajili kukidhi mahitaji yake ya kila siku kama vile mavazi malazi na chakula.Shughuli hizo ni pamoja na kilimo,Ufugaji,Uvuvi,Uchimbaji Madini,na shughuli zingine ambazo zinamuwezesha kumuingizia kipato cha kila siku.Tume ya Maendeleo kupitia Wizara ya Kilimo kwa kutambua umuhimu wa shughuli zinazofanywa na wanajamiii wake wakaamua kuanzisha Ushirika ili kuwaweka watu pamoja ili waweze kujikwamua na kupata faida zitokanazo na Ushirika.

Tunaweza kujiuliza maana halisi ya Ushirika ni ipi? Ushirika ni muungano wa watu ambao wanafanya kazi pamoja kwa hiari ilikufanikisha mahitaji yao ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kupitia shughuli inayomilikiwa kwa pamoja na kudhibitiwa kidemokrasia. Ushirika unazingatia maadili ya kujisaidia wenyewe, jukumu binafsi, demokrasia, usawa na mshikamano. Wanachama wa ushirika wanaamini katika uaminifu, uwazi, uwajibikaji kwa jamii na kuwajali wengine.

Sasa tuangalie na kufahamu ni upi umuhimu wa vya Ushirika? Umuhimu mkubwa wa vyama hivi vya ushirika ni kuhakikisha kuwa vinamkwamua mwanaushirika na kuinua hali yake yakimaisha, pia kutoa huduma kwa wanachama wake yakiwemo mahitaji ya pembejeo za kilimo,kupata mikopo kwa njia rahisi,kukusanya na kusindika na kiutafuta masoko ya bidhaa za wanachama wake.

Katika kuhakikisha Ushirika unakuwa imara na kuweza kuaminiwa na kila mwanaushirika,basi viongozi kwa kushirikiana na wanaushirika huandaa majukwaa ya Ushirika ambayo lengo kuu huwa ni kufanya tathmini ya shughuli zinazofanywa na Vyama vya Ushirika na kupanga mikakati kwaajili ya mwaka mzima unaofuata pamoja na maboresho zaidi, hivyo basi kila mkoa ambao una vyama vya Ushirika huandaa Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika ikiwa pia ni maandalizi ya Siku ya Ushirika Duniani.

Kama ilivyo maana ya Ushirika Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kushirikiana na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) na Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU) iliratibu maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD) - 2023 yaliyofanyika kitaifa kuanzia tarehe 26/06/2023 hadi tarehe 01/07/2023 Mkoani Tabora katika Viwanja vya Nanenane – Ipuli Mkoani Tabora.

Lengo la maadhimisho hayo ikiwa ni kuwakutanisha Wadau wa Ushirika wakiwemo Viongozi wa Ushirika, Vyama vya Ushirika, Wadau wa Ushirika na Viongozi wa Serikali

wanaosimamia Sekta ya Ushirika kutangaza kazi za wanaushirika, kuhabarisha Umma juu ya falsafa na manufaa ya Ushirika na kutoa fursa ya kujadili changamoto za kiuchumi na kijamii zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi.

Kwa mwaka huu 2023;Maadhimisho hayo yaliambatana na shughuli mbalimbali ikiwemo makongamano, utoaji wa zawadi, Uchangiaji Damu, Upimaji wa Afya, Shindano la insha, makongamano ya elimu ya Ushirika,utoaji wa tuzo za utambuzi wa mchango kwa Vyama,watendaji,wadau,waandishi wa Habari na tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika Uandishi wa Insha za Ushirika pamoja Burudani na Michezo.

Maadhimisho yalitoa nafasi ya kuonesha bidhaa za Wanaushirika, Kazi za Wanaushirika na kuuenzi Ushirika ili kufanikisha Ajenda ya Kimataifa - 2030 na Malengo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDGs) kupitia Ushirika. Hata hivyo katika maadhimisho ya mwaka huu tukio kubwa lilikuwa ni uzinduzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ujulikanao kama MUVU.

Waziri wa kilimo Mhe. Hussein Bashe katika kilele cha Maadhimisho hayo alizindua rasmi Mfumo huo na kutoa maelekezo kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuwa Mfumo wa MUVU uunganishwe na Mifumo mingine ili kuimarisha na kuboresha sekta ya Ushirika.

"Mfumo huu uonane na mifumo mingine kama ule wa kusajili wakulima wa nchi nzima, tuwe na Mfumo mmoja na utaonyesha miamala za Mkulima za kila siku," alisema Mhe. Bashe.

Katika Maadhimisho ya mwaka huu, Wanaushirika walipata fursa ya kutekeleza Msingi Namba 7 wa Ushirika wa kuijali jamii kwa washiriki wote kushiriki katika utoaji wa misaada na mahitaji kwa wahitaji, kama vile Yatima, Wagonjwa hospitalini; ushiriki katika upimaji afya na uchangiaji damu pamoja na kushiriki katika michezo mbalimbali.

Vilevile, Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yalitoa fursa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kutoa huduma kwa washiriki na kupelekea kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, uchumi wa Mkoa husika na Taifa kwa ujumla, pamoja na kutoa fursa kwa wadau wa Maendeleo ya Ushirika kujifunza kuhusu fursa za uwekezaji na biashara kupitia bidhaa na mazao yanayozalishwa kwenye Vyama vya Ushirika.

Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yamesaidia kuwaunganisha wanaushirika na Wabia wa Maendeleo toka ndani na nje ya nchi na kuviunganisha Vyama vya Ushirika ili kuimarisha mahusiano katika kusaidiana masuala ya kiuchumi na kijamii.

Aidha, Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yamesaidia washiriki mbalimbali kupata fursa za kielimu sambasamba na kubadilishana uzoefu kupitia makongamano mbalimbali wakati wa maadhimisho na hutoa fursa kwa Vyama vya Ushirika na Wadau wa Maendeleo ya Ushirika kubadilishana uzoefu, mbinu za usimamizi, ubunifu na mtandao wa masoko.

*HABARI PICHA*














# HABARI PICHA










Corporate
Governance


KCBL
KILIMANJARO
CO-OPERATIVE BANK
LIMITED
Together, Transforming Lives
WELCOME TO THE BANKERS'
AWARDS AND GALA DINNER 2023
TRAINING SOLUTIONS
KCBL BANK
WINNERS
2023
TANZANIAN BANKER$ CHALLENGE



•

## MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA YA MFUMO WA MUVU

1. **Je, nawezaje kupata "Mwongozo wa jinsi ya kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Vyama Vya Ushirika- MUVU ".?**

**Jibu**: Mwongozo wa jinsi ya kutumia Mfumo wa MUVU unapatikana kwenye Tovuti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kupitia anwani ya www.ushirika.go.tz, kwenye menu ya **Machapisho kipengere** kidogo cha **Miongozo**

2. **Je, nawezaje kupata "Mwongozo wa Matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara".?**

**Jibu**: Kwa kupitia tovuti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika www.ushirika.go.tz, kipengele cha **Machapisho** kisha kipengele kidogo cha **Miongozo.**

3. **Je, nifanyeje ninapotuma Makisio ya Mapato na Matumizi ya Chama, ninapo pata tatizo (error message) inayosema "*Estimated development amount exceeds budget*" wakati wa kujaza bajeti ya Maendeleo.?**

**Jibu**: Hakikisha unapojaza bajeti yako ya Maendeleo (**Development Budget**), Jumla ya Mapato kwenye "development budget" haizidi kiwango cha bakaa yako ya **Mapato na Matumizi (Surplus Amount)** ambayo inapatika kwenye Taarifa yako ya Mapato na Matumizi kitufe cha "**View Estimate Summary**".

Na kama Chama kina Mkopo kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo (**Loan for Development Budget**) kabla ya kujaza Bajeti ya Maendeleo, hakikisha unajaza ***kasma*** hiyo iliyopo kwenye Taarifa ya Makisio ya Mapato na Matumizi, kipengele kilichoandikwa "**Loan for Development Budget/Mkopo kwa ajili ya shughuli za Maendeleo"**

4. **Je, nifanyeje ninapopata tatizo wakati wa kusajili Wanachama kwa kutumia "*Excel*".?**

**Jibu**: Hakikisha kwanza umepakua "**Template"** kwenye Mfumo wa **MUVU** sehemu ya **taarifa za wanachama** kwa wanachama na "**Template**" ya **taarifa za wasio wanachama** sehemu ya Taarifa za wasio Wanachama ukiwa kwenye akaunti ya Chama cha Ushirika

5. **Wakati wa kujaza Taarifa ya Mkopo wa Pembejeo (Agricultural Input Loan) napata ujumbe huu "*Loan amount exceeds estimated amount! OR May-be you don't have any Agricultural Input Estimate". Tatizo ni nini?***

**Jibu**: Kabla ya kujaza Taarifa za mkopo husika, hakikisha umejaza taarifa ya Makadirio ya Mkopo wa Pembejeo (**Agricultural Inputs Loan Estimate**) kwa kuchanganua pembejeo zote zinazohitajika na Wanachama, kwa kupitia kwenye kitufe cha "**Add Agricultural Input Estimate**" kwenye Taarifa yako ya Makisio ya Mapato na Matumizi.

6. **Wakati wa kutuma na kujaza Taarifa ya Makisio ya Mapato na Matumizi ya Chama, Napata ujumbe huu "*You don't have a Previously Financial Report" kwa upande wa SACCOS, nifanyeje?***

> **Jibu**: Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (**SACCOS**) ambacho sio kipya, kabla ya kutuma taarifa za Makisio ya Mapato na Matumizi kihakikishe kimewasilisha kupitia kwenye Mfumo wa MUVU **Taarifa za Utendaji wa Fedha (Financial Performance)** ya Mwaka wa nyuma (**Previously Year)**

7. **Napata shida wakati wa kuomba, Bajeti ya Nyongeza (Supplimentary Budget) au Ukomo wa Madeni baada ya Makisio ya Mapato na Matumizi ya Chama,baada ya Mapato na Matumizi chama kuwa yalishaidhinishwa**

> **Jibu**: Hakikisha Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Chama kwa mwaka husika inaonyesha **"status"** ya "Approved", kisha utabonyeza kitufe kilichoandikwa "**Request Supplimentary Budget"** kwa ajili ya kuomba Bajeti ya Nyongeza na kitufe kilichoandikwa **"Add Loan"** kwa ajili ya kuomba Ukomo wa Madeni.

8. **Wakati wa kuingiza Taarifa za kiutendaji za Utendaji wa Fedha (Financial Performance) za kila mwezi/Robo zinagoma, nifanyeje?**

> **Jibu**: Hakikisha kwanza unajaza Fomu ya Mapato na Matumizi (***Comprehensive Income***) kisha jaza Fomu ya **Mizania ya Fedha (*Financial Position), alafu endelelea na fomu zinazofuata***

9. **Nikiingiza email yangu na password napata ujumbe huu *"Invalid username or password"* nifanyeje?**

> **Jibu**: Hakikisha Taarifa za akaunti yako "**username na nywila zipo sahihi na v**imesajiliwa kwenye Mfumo wa MUVU. Kama bado wasiliana na **Afisa Ushirika wa Halmashauri** yako au **Mrajis Msadizi wa Mkoa** kwa msaada**.**

10. **Naomba kujua utarartibu wa kukusanya *mazao na mauzo* ya wakulima kwa upande wa Chama cha Ushirika na Chama Kikuu**.?

> **Jibu**: Ukiwa kwenye **Mfumo wa MUVU**, kwenye menu ya ***Masoko na Uwekezaji,*** nenda sehemu ya **"Makusanyo/Stock Balance"** weka taarifa ya **Mauzo ya mazao** kwa msimu husika, kisha baada ya kukusanya tengeneza latalogi, baada ya katalogi changua aina ya kuuza (Mnada, Direct au kilimo cha Mkataba) endelea nah atua za mauzo kwa kubonyeza

11. **Naomba kujua jinsi ya kuandaa na kuwasilisha Taarifa za *Mikataba na Randama za Makubaliano* kwa upande wa Chama cha Ushirika?**

**Jibu**: Ukiwa kwenye **Mfumo wa MUVU**, kwenye ***menu*** ya **Mikata na Randama za Makubaliano**, ukibonyeza itakupa sehemu inayoonesha maeneo ya kujaza wakati taarifa za mikataba inayoingiwa na Chama cha Ushirika, kwa kwenda sehemu iliyoandikwa

- *Kwa maelezo zaidi kuhusu Mfumo wa* **Usimamizi wa Vyama vya Ushirika***, **pakua*** **Mwongozo wa Mtumiaji wa Mfumo wa Vyama vya Ushirika (User Manual)** *pamoja na* **Mwongozo wa Matumizi ya Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika** *kupitia kwenye tovuti ya Tume,* https://www.ushirika.go.tz